


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA MAMBO YA NJE  
NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA



Hotuba ya Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe (Mb),  
Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa akiwasilisha Bungeni  
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa  
kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.



Hotuba ya Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe (Mb), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

## **YALIYOMO**

<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
<b>TATHMINI YA HALI YA DUNIA.....</b>	<b>5</b>
Hali ya Maendeleo Duniani .....	5
Hali ya Amani Barani Afrika.....	6
Burundi .....	6
Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).....	8
Libya .....	9
Hali ya Kisiasa Mashariki ya Kati.....	10
Kuibuka na Kushamiri kwa Vikundi vya Kigaidi.....	11
<b>UHUSIANO WA TANZANIA NA NCHI JIRANI.....</b>	<b>12</b>
Chaguzi za Nchi za Afrika na wajibu wa Watanzania kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba 2015.....	13
<b>MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MASUALA MUHIMU YA KIMATAIFA.....</b>	<b>14</b>
Sudan Kusini .....	14
Mpaka baina ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa .....	15
Mgogoro wa Saharawi .....	16
Mgogoro kati ya Palestina na Israel .....	17
Mpango wa Nyuklia wa Iran .....	17
Uhusiano kati ya Cuba na Marekani .....	18
Mgogoro wa Ukraine.....	18
<b>MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA AWAMU YA NNE.....</b>	<b>19</b>
<b>UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.....</b>	<b>22</b>
<b>USHIRIKIANO WA KIMATAIFA .....</b>	<b>22</b>
Kikao cha 69 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA).....	22
Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs)	

na Ajenda ya Maendeleo baada ya Mwaka 2015 (P2015DA).....	23
Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi .....	24
Mkutano wa Kimataifa kuhusu Biashara Haramu ya Wanyamapori .....	25
<b>ULINZI NA UJENZI WA AMANI DUNIANI .....</b>	<b>26</b>
<b>USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA UMOJA WA AFRIKA NA JUMUIYA ZA KIKANDA .....</b>	<b>27</b>
Umoja wa Afrika .....	27
Uenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi ( <i>Committee of African Heads of State and     Government on Climate Change-CAHOSCC</i> ) .....	28
Umoja wa Afrika Kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere .....	28
Watanzania kushika nyadhifa mbalimbali katika Taasisi za Umoja wa Afrika.....	29
Nafasi ya Tanzania katika Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika.....	29
Jumuiya ya Afrika Mashariki .....	30
Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) .....	31
Jumuiya ya Nchi zilizo katika Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) .....	32
Jumuiya ya Nchi zilizo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA).....	32
Maandalizi ya uzinduzi wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA - EAC - SADC (COMESA - EAC - SADC Tripartite Free Trade Area).....	32
<b>KUSIMAMIA MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA .....</b>	<b>33</b>
<b>WATANZANIA WAISHIO UGHAIBUNI (DIASPORA) .....</b>	<b>34</b>
<b>MASUALA YA DIPLOMASIA, ITIFAKI, UWAKILISHI NA HUDUMA ZA KIKONSELI.....</b>	<b>36</b>
<b>MASHAMBULIZI YA WAGENI NCHINI AFRIKA KUSINI.....</b>	<b>38</b>
<b>MCHANGO WA WIZARA KWENYE SEKTA MBALIMBALI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 .....</b>	<b>39</b>
Sekta ya Elimu.....	40

Sekta ya Afya .....	40
Sekta ya Maji .....	41
Sekta ya Viwanda .....	42
Sekta ya Maliasili na Utalii .....	42
Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.....	43
Sekta ya Uchukuzi .....	44
Biashara na Uwekezaji .....	45
Sekta ya Ajira.....	46
<b>UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI WIZARANI NA BALOZINI.....</b>	<b>47</b>
Mafunzo ya Watumishi .....	47
Uteuzi wa Viongozi .....	48
Kuwarejesha nchini Watumishi waliomaliza muda wao nje.....	48
Mkutano wa Nne wa Mabalazi wa Tanzania.....	49
<b>TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA .....</b>	<b>50</b>
Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM) .....	51
Mafanikio ya Utekelezaji wa APRM.....	51
Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) 2015/16 .....	52
<b>MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 .....</b>	<b>53</b>
<b>CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 .....</b>	<b>54</b>
<b>MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 .....</b>	<b>56</b>
<b>MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016.....</b>	<b>57</b>
<b>HITIMISHO .....</b>	<b>58</b>

## Orodha ya Vifupisho

---

ADF	Allied Democratic Forces
AICC	Arusha International Conference Centre
APRM	African Peer Review Mechanism
AUABC	African Union Advisory Board on Corruption
BADEA	Arab Bank for Economic Development in Africa
BRN	Big Results Now
CNDD-FDD	The National Council for the Defense of Democracy – Forces for the Defense of Democracy
CMHI	China Merchants Holding international
CFR	Mozambique-Tanzania Centre for Foreign Relations
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Africa
SGRF	State General Reserve Fund
EAC	East African Community
DRC	The Democratic Republic of the Congo
GDP	Growth Domestic Product
LAPF	Local Authorities Pension Fund
MDGs	Millennium Development Goals
MoU	Memorandum of Understanding
NIDA	National Identification Authority
NPoA	National Programme of Action
NSSF	National Social Security Fund
PAC	Public Accounts Committee
PSPF	Public Service Pensions Fund
PPF	Parastatal Pension Fund
SDGs	Sustainable Development Goals
TDI	Tanzania Diaspora Initiative

TIC	Tanzania Investment Centre
MONUSCO	United Nations Organization Stabilization Mission in the DRC
ICGLR	International Conference on the Great Lakes Region
IOM	International Organization for Migration
IORA	Indian Ocean Rim Association
FDLR	Democratic Forces for the Liberation of Rwanda
IS	Islamic State
MOJWA	The Movement for the Oneness and Jihad in West Africa
UN	United Nations
AU	African Union
CCM	Chama Cha Mapinduzi
SPLM	Sudan People's Liberation Movement
ANC	African National Congress
IGAD	Intergovernmental Authority on Development
EU	European Union
UAE	United Arab Emirates
JWTZ	Jeshi la Wananchi Tanzania
UNAMID	African Union/United Nations Hybrid Operation in Darfur
UN-Habitat	United Nations Human Settlements Programme
WHO	World Health Organization
FAO	Food and Agriculture Organization
UNGA	United Nations General Assembly
UNISFA	United Nations Interim Security Forces for Abyei
UNFIL	United Nations Interim Force in Lebanon
UNOC	United Nations Operation in the Congo
UNMISS	United Nations Mission in the Republic of South Sudan
OAU	Organisation of African Unity



## Utangulizi

1. ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.
2. ***Mheshimiwa Spika***, kwanza kabisa, naungana na Wabunge wenzangu walionitangulia kutoa salamu za pole na rambirambi kwako na kwa familia ya marehemu Kapteni John Damiano Komba aliyekuwa Mbunge wa Mbinga Magharibi na wananchi wote wa Jimbo hilo kwa msiba mkubwa na wa ghafla wa kuondokewa na Kiongozi wao na Mbunge mwenzetu. Kadhalika, napenda kutoa pole kwa familia ya Mwalimu Nyerere kwa kuondokewa na kijana wao mpendwa Bw. John Nyerere ambaye alitoa mchango mkubwa kwa nchi yetu wakati wa vita ya Kagera. Vilevile, nitoe pole kwa Wizara na familia za watumishi wenzetu wawili, Bw. Mohammed Kombo na Bi. Emerentiana Shirima, ambao walifikwa na mauti wakati wakiendelea kuitumikia Wizara na Taifa kwa ujumla. Tuendelee kuwaomba kwa Mwenyezi Mungu awapumzishe kwa amani. Amina.
3. ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 26 Aprili, 2015 wakati tukiadhimisha miaka 51 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Tanzania ilipoteza nuru ya ukombozi wa Bara la Afrika, Marehemu Balozi Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hashim Mbita. Marehemu Mbita aliyewahi kuwa Katibu wa Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika alikuwa ni kiungo muhimu kati ya Tanzania na nchi zilizokuwa zinapigania uhuru wake zikiwemo Angola, Shelisheli, Namibia, Zimbabwe, Msumbiji na Afrika Kusini. Harakati hizo za ukombozi zimejengea Tanzania sifa na heshima kubwa Ulimwenguni.

4. ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuhakikisha kumbukumbu na historia ya harakati za kupigania uhuru zinatunzwa, Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika Gaborone, Botswana mwezi Agosti 2005, ulimtaka Marehemu Balozi Brigedia Jenerali Hashim Mbita kusimamia Mradi wa Ukusanyaji wa Kumbukumbu hizo uliojulikana kama “*Hashim Mbita Research Project*”. Vitabu vilivyobeba kumbukumbu hizo, vilizinduliwa rasmi katika Mkutano wa 34 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC mwezi Agosti 2014, huko Victoria Falls, Zimbabwe. Naungana na wananchi wenzangu kutoa pole kwa familia ya marehemu Balozi Brigedia Jenerali (Mstaafu) Hashim Mbita. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.
  
5. ***Mheshimiwa Spika***, kwa masikitiko makubwa nitoe mkono wa pole kwa ndugu, jamaa na rafiki zetu wenye Ulemavu wa Ngozi (Albinism) kwa madhila waliyofanyiwa yakiwemo ya kukatwa kwa viungo vyao vya mwili na hata kuuawa. Tunawaombea ndugu, jamaa na marafiki wa familia hizo ili Mungu azidi kuwatia nguvu na faraja katika kipindi hiki kigumu. Kadhalika, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Serikali kwa ujumla kukemea vikali vitendo vya mauaji na ukatili vinavyofanywa na watu wachache wenye imani potofu dhidi ya wenzetu hawa. Vitendo hivi si tu vinaidhalilisha na kuifedhehesha nchi yetu bali pia vinakiuka misingi mikuu ya haki za binadamu. Hapana shaka taswira nzuri ya nchi yetu iliyodumu kwa miongo mitano (5) tangu tupate uhuru wetu imechafuliwa sana na vitendo viovu vya wenzetu wachache. Ndugu Watanzania wenzangu, nawaombeni tuendelee kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha na uhalifu huu ambao unachafua taswira ya nchi yetu inayojulikana kuwa kitovu cha amani duniani.

6. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia nitumie nafasi hii adhimu kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniadini na kunitua kuwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa takriban miaka nane na nusu mfululizo. Jukumu hili halikuwa rahisi, lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, miongozo ya mara kwa mara ya Mheshimiwa Rais, maoni ya Wabunge na Mawaziri wenzangu, niliweza kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia Sera ya Mambo ya Nje kwa ufanisi katika kipindi chote hicho na kuifanya Tanzania kung'ara katika medani za Kimataifa.
  
7. *Mheshimiwa Spika*, nampongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Ni dhahiri kuwa, kutokana na umahiri wake huo katika uongozi hususan kwenye medani za Kimataifa, haikunishangaza mimi binafsi na Watanzania kwa ujumla kuona Mheshimiwa Rais akikasimiwa majukumu mbalimbali ya Kimataifa. Mathalan, mwezi Machi 2015, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Ban Ki Moon, alimteua Rais Kikwete kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Watu Mashuhuri Kushughulikia Majanga ya Kiafya Duniani (*The Chairman of the United Nations High Level Panel on the Global Response to Health Crisis*).
  
8. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Mei 2015, Jopo hilo lilikutana kwa mara ya kwanza New York, Marekani ambapo lilitengeneza ratiba ya kutekeleza majukumu yake. Kwa kuanzia, Jopo hilo limepanga kutembelea maeneo yaliyoathirika na Ebola na kutoa mapendekezo ya namna ya kushughulikia majanga ya aina hiyo.
  
9. *Mheshimiwa Spika*, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa watoa hoja waliozungumza kabla yangu hususan Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb), Waziri wa Fedha; na Mheshimiwa Mary Nagu

(Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uhusiano na Uratibu kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa dira na zimegusia kwa ufasaha masuala mbalimbali muhimu ya Kitaifa na Kimataifa na yale yanayoigusa Wizara yangu moja kwa moja. Pia, nawashukuru Mawaziri wengine wote walionitangulia kwa hotuba zao zenye kutoa mwanga wa maendeleo kwa Watanzania katika mwaka ujao wa fedha.

10. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Makamu wake, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri, maoni na maelekezo yao ambayo kwa kipindi chote yamekuwa ni msaada mkubwa kwa Wizara yangu katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje. Kamati hiyo ilitoa mchango mkubwa kwa Wizara kuanza kutekeleza Mpango wa Ununuzi wa Majengo ya Makazi ya Watumishi na ofisi katika balozi za Tanzania. Mpango huo, umesaidia kwa kiwango kikubwa kuipunguzia Wizara mzigo wa kulipa pango za majengo ya ofisi na makazi.
  
11. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwashukuru kwa dhati Wafanyakazi wote wa Wizara waliopo Makao Makuu, Ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar, Balozi za Tanzania na Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dkt. Mahadhi Juma Maalim (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Katibu Mkuu, Balozi Hassan Simba Yahya, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Mabalozzi, na Wakuu wa Vitengo kwa ushauri na utayari wao wakati wote katika kunisaidia kutekeleza majukumu yangu ya msingi ya kutetea maslahi ya Taifa letu.

12. *Mheshimiwa Spika*, naomba nitumie nafasi hii kwa namna ya pekee kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtama kwa kuniamini na kunikubali kuwatumikia katika kipindi cha miaka kumi na tano (15). Uaminifu wao umekuwa ni nguvu kubwa kwangu ya kuniwezesha kusonga mbele na hata kufikia hatua hii niliyopo sasa. Aidha, namshukuru kwa dhati Mke wangu Mama Dorcas Membe, Watoto na familia yangu yote kwa ujumla kwa uvumilivu wao na kuwa karibu na mimi wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu ambayo kwa kiasi fulani yalinilazimu kuwa mbali nao kwa vipindi virefu.
13. *Mheshimiwa Spika*, naomba pia nitoe pongezi zangu kwa Wabunge wapya wawili waliojiunga nasi hivi karibuni. Wabunge hao ni Mheshimiwa Dkt. Grace Khwaya Puja (Mb) na Mheshimiwa Innocent Rwabushaija Sebba (Mb). Nawapongeza sana kwa kuteuliwa na kuwa sehemu ya Bunge hili.

## TATHMINI YA HALI YA DUNIA

### Hali ya Maendeleo Duniani

14. *Mheshimiwa Spika*, hali ya uchumi wa dunia inaendelea kuimarika kufuatia jitihada zilizofanywa za kukabiliana na kudorora kwa uchumi. Hata hivyo, kuimarika huko kwa uchumi hakujasadifu hali halisi ya maisha ya watu wa kawaida katika maeneo mbalimbali duniani ikiwemo Tanzania, hivyo, ongezeko hilo halijasaidia kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa.
15. *Mheshimiwa Spika*, dunia inashuhudia kuporomoka kwa bei ya mafuta ghafi kwenye soko la dunia kutokana na sababu mbalimbali. Anguko hilo la bei ya mafuta limekuwa ni ahueni kwa nchi zinazotegemea nishati hiyo kwa uzalishaji. Hata hivyo, sio taarifa njema kwa nchi zinazozalisha na zinazoendelea na utafiti wa mafuta na gesi kwani inaweza kuathiri uwekezaji kwenye sekta ya mafuta na gesi katika nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania.

16. *Mheshimiwa Spika*, ni wazi kwamba, hali hii ya uchumi wa dunia imeathiri utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) ambao utafikia mwisho ifikapo mwezi Septemba 2015. Yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa baadhi ya malengo, lakini pia yapo malengo ambayo utekelezaji wake hautakamilika na hivyo kurithiwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) yatakayojumuishwa kwenye Ajenda ya Maendeleo baada ya 2015. Baadhi ya maeneo ambayo Tanzania imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwenye utekelezaji wa Malengo ya Milenia ni kupunguza vifo vya mama na mtoto, kupunguza ugonjwa wa Malaria Zanzibar, kupunguza maambukizi mapya ya ugonjwa wa UKIMWI, kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi mbalimbali za maamuzi, na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa katika elimu ya msingi.

## **Hali ya Amani Barani Afrika**

17. *Mheshimiwa Spika*, hali ya amani na usalama Barani Afrika kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 imezidi kuimarika. Jitihada zinaendelea ili kutafuta suluhu ya migogoro ya kisiasa inayoendelea kwenye nchi kama Sudan Kusini, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

## **Burundi**

18. *Mheshimiwa Spika*, takriban kwa kipindi cha miezi miwili sasa, hali ya kisiasa nchini Burundi imeendelea kudorora kufuatia uamuzi wa chama tawala cha CNDD-FDD kumtangaza Mheshimiwa Pierre Nkurunziza, Rais wa Jamhuri ya Burundi kugombea nafasi ya Urais wa nchi hiyo katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika tarehe 26 Juni, 2015. Uamuzi huo ulipelekea kuwepo kwa vurugu na maandamano makubwa katika mji mkuu wa Bujumbura na maeneo ya jirani na hivyo kusababisha vifo vya watu na uharibifu wa mali na wengine kuikimbia nchi yao. Hali ilizidi kuwa tete baada ya uamuzi wa Mahakama ya Katiba nchini humo kuridhia Rais Nkurunziza kugombea tena katika uchaguzi huo.

19. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 6 Mei, 2015 Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), alinituma kuongoza ujumbe maalumu wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Jumuiya hiyo kwenda nchini Burundi kwa ajili ya kufanya tathmini ya hali halisi ya kisiasa, kiulnzi na kiusalama. Wakati wa ziara hiyo tulikutana na kufanya mazungumzo na Rais Pierre Nkurunziza na baadae viongozi wa vyama 43 vya siasa nchini humo. Ujumbe huo, ulibaini kuwepo kwa hali tete ya usalama, na kuwepo kwa chuki na maandamano ya kuipinga Serikali ya Burundi, hasa Bujumbura. Hadi tunaondoka Bujumbura, watu 600 walikuwa wamewekwa rumande, 8 kuuawa na zaidi ya 50,000 kukimbilia nchi za Rwanda na Tanzania.
20. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 13 Mei, 2015 Rais Kikwete aliitisha Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa EAC mara baada ya kupokea taarifa hiyo ya Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Jumuiya hiyo kwa lengo la kujadili hali ya kisiasa na usalama nchini Burundi. Wakati Mkutano unaendelea, kulitokea jaribio lililoshindwa la kutaka kuipindua Serikali ya Rais Nkurunziza. Katika jaribio hilo, gereza lilivunjwa na wafungwa wote kuachiliwa, maandamano mjini Bujumbura yalikuwa makubwa na ya fujo, mawasiliano yalikatwa na vituo vya habari kuchomwa moto, watu wapatao laki moja walikimbilia nchi jirani za Rwanda na Tanzania. Viongozi wote wa Jumuiya walilaani vikali jaribio hilo.
21. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania, kama Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na muhanga mkubwa wa machafuko yanayotokea katika ukanda wa Maziwa Makuu, tutaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kutafuta suluhu kwa lengo la kuhakikisha kuwa amani inarejea nchini Burundi ili kuwezesha Uchaguzi Mkuu ulio huru, wa haki, amani na utulivu.

## **Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)**

- 22.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya kipigo cha M23 cha mwaka 2014, hali ya ulinzi na usalama katika eneo la Maziwa Makuu hususan katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) inaendelea kuimarika. Hata hivyo, makundi ya uasi kutoka nje ya DRC kama Allied Democratic Forces (ADF) na FDLR yanaendelea kuleta changamoto hususan mashariki mwa DRC. Majeshi yetu ambayo yamefanya kazi kubwa inayotujengea heshima kubwa Duniani, sasa yamepata jukumu la kuwashughulikia ADF (waasi wa Uganda ambao wanaivuruga Uganda kutokea DRC). Sambamba na hilo waasi wa FDLR wanashughulikiwa na majeshi ya Afrika Kusini na Malawi.
- 23.** *Mheshimiwa Spika*, hata hivyo, changamoto iliyopo ni kutokukubaliana kati ya Serikali ya DRC na MONUSCO kuhusu uteuzi wa Mabrigedia wawili wanaoongoza vikosi vya DRC ambao wanatuhumiwa kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.
- 24.** *Mheshimiwa Spika*, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Mkutano wa Pamoja wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC na ICGLR uliofanyika Angola mwezi Juni 2014 uliamua kwamba kundi la FDLR wapewe kipindi cha miezi sita kuanzia tarehe 2 Julai 2014 hadi tarehe 2 Januari 2015 kuweka chini silaha zao kwa hiari vinginevyo lingeshurutishwa kufanya hivyo. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Januari 2015 kundi hilo halikuweza kutekeleza amri hiyo. MONUSCO pamoja na Umoja wa Mataifa ukaamua kuwa FDLR na ADF zishughulikiwe kama M23 walivyoshughulikiwa. Tanzania ipo tayari na majeshi yetu yapo kazini. Napenda kuchukuwa nafasi hii kutoa salamu za pole kwa familia za askari wetu wawili waliopoteza maisha hivi karibuni wakati wakitekeleza majukumu yao dhidi ya waasi wa ADF huko mashariki mwa DRC. Napenda



kuwafahamisha Watanzania wenzangu kwamba hakuna damu ya mashujaa wetu hao itakayopotea bure katika uwanja wa mapambano. Ipo gharama itakayolipwa na wale waliosababisha damu ya askari wetu kumwagika. Kama bado haijalipwa.

## **Libya**

25. *Mbeshimiwa Spika*, hali ya kiusalama nchini Libya imeendelea kudorora tangu kuuawa kwa aliyekuwa Kiongozi wa nchi hiyo Kanali Muammar Gaddafi na Serikali yake kupinduliwa. Kutokuwepo kwa Serikali imara nchini Libya kumepelekea kuongezeka kwa vitendo vya kigaidi pamoja na kutoa mwanya kwa makundi ya Al-Qaeda na IS kufanya shughuli zake nchini humo.
  
26. *Mbeshimiwa Spika*, mnamo mwezi Februari 2015 Umoja wa Mataifa uliongoza mazungumzo ya kutafuta suluhu ya mgogoro huo mjini Ghadames, Libya ambayo yalifuatiwa na mazungumzo mengine yaliyohusisha pande zinazohasimiana mjini Skhirat, Morocco, mwezi Machi 2015. Lengo la mazungumzo hayo lilikuwa ni kuanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa pamoja na kuandaa taratibu za kumaliza kuandika Katiba ya nchi hiyo. Hata hivyo, juhudi hizo za Jumuiya ya Kimataifa bado hazijaweza kuzaa matunda na nchi hiyo hivi sasa inaendeshwa na Serikali mbili zinazopingana.
  
27. *Mbeshimiwa Spika*, Tanzania ililaani vikali matumizi ya nguvu kuuondoa uongozi uliokuwa madarakani pamoja na mauaji ya Kanali Muammar Gaddafi aliyekuwa kiongozi wa Libya, msimamo ambao bado haujabadilika. Tanzania inaendelea kuzisihi pande zote zinazopingana kutafuta suluhu ya kudumu kwa njia ya mazungumzo. Tunaamini kuwa mazungumzo ndiyo njia pekee itakayoifanya Libya si tu kuwa na Serikali imara bali pia yenye ridhaa ya Walibya wote.

## Hali ya Kisiasa Mashariki ya Kati

28. *Mheshimiwa Spika*, hali ya amani na usalama katika eneo la Mashariki ya Kati imeendelea kuzorota hasa baada ya wimbi la baadhi ya makundi kuanzisha vurugu na vita kwa madai ya demokrasia na utawala wa sheria katika nchi za kiarabu. Hali hiyo, imechochea kasi ya kutaka kuwaondoa madarakani viongozi waliopo na kuwaweka wanaodaiwa kuhubiri demokrasia. Matokeo yake ni kuzaliwa kwa makundi mengi yenye misimamo mikali ya kigaidi.
  
29. *Mheshimiwa Spika*, moja ya makundi hayo ni lile linalojiita wapiganaji wa Dola ya Kiislam yaani *Islamic State* (IS) ambalo linaendesha mapambano nchini Syria na Iraq likiwa na lengo la kuunda Dola ya Kiislamu ikianza Iraq hadi Syria. IS imeanza kuwa na ushawishi kwa makundi mengine ya kigaidi kama vile Boko Haram la Nigeria na Al-Shaabab la Somalia ambayo yanajitangaza kuwa wafuasi wa Itikadi ya kundi hilo.
  
30. *Mheshimiwa Spika*, sote tumeshuhudia kupitia vyombo vya habari unyama unaotendwa na kundi hili kwa kuua watu wasiokuwa na hatia na hasa kwa kuwakata vichwa. Hali hii inalifanya kundi hilo kuwa ni tishio, sio tu kwa Syria na mataifa mengine ya Mashariki ya Kati bali dunia nzima kwa ujumla na limefanya mgogoro wa Syria uliodumu zaidi ya miaka minne kuwa mgumu kupata suluhu. Jumuiya ya Kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa lazima ifanye kila linalowezezana kurejesha amani nchini Syria na maeneo yote ambayo kundi hilo linafanya uhalifu.
  
31. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Yemen, tumeshuhudia machafuko ya vita ya wenyewe kwa wenyewe ambapo wapiganaji wa kikundi cha Houthi wamekuwa katika mapigano na Majeshi ya Serikali. Mapigano hayo yamepelekea nchi za Ghuba zikiongozwa na Saudi Arabia kuisaidia Serikali ya Yemen kupigana na waasi hao kitendo ambacho kinapingwa vikali na Serikali ya Iran.

32. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inaunga mkono juhudi za Jumuiya ya Kimataifa za kutafuta suluhu ya kudumu kwenye mgogoro huo, kwa njia ya amani. Tunaamini kuwa matumizi ya nguvu za kijeshi hayawezi kuleta suluhu ya kudumu ya mgogoro huo bila kuwa na madhara makubwa kwa usalama na uchumi wa wananchi wa Yemen.

### **Kuibuka na Kushamiri kwa Vikundi vya Kigaidi**

33. *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyoeleza kuhusu hali ya kisiasa Mashariki ya Kati, dunia imeendelea kushuhudia kuibuka na kuimarika kwa vikundi mbalimbali vya kigaidi. Makundi hayo ya kigaidi kama vile Islamic State (IS), Al-Shaabab, Boko Haram, Al-Qaeda in the Gulf of Yemen and The Islamic Maghreb, Ansaru na The Movement for the Oneness and Jihad in West Africa (MOJWA), yamechangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kwa hali ya usalama na amani duniani.
34. *Mheshimiwa Spika*, taarifa ya Jopo la Wataalam wa Umoja wa Mataifa kuhusu vikwazo dhidi ya Al-Qaeda (*The Pannel of Experts Monitoring the UN Sanctions Against Al-Qaeda*) iliyotolewa mwezi Machi 2015 inaonyesha kuwa idadi ya wapiganaji wa kigeni wanaojiunga na makundi ya kigaidi imeongezeka kwa zaidi ya asilimia 71 kutoka mwaka 2014 hadi 2015. Inakadiriwa kuwa katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, idadi ya wapiganaji wa kigeni wanaojiunga na makundi hayo ni zaidi ya 25,000.
35. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha hivi karibuni, Afrika imeshuhudia matukio mbalimbali ya kigaidi yaliyosababisha kuzorota kwa hali ya amani na usalama. Matukio kama ya kutekwa kwa wanafunzi wa kike nchini Nigeria, mashambulizi ya kundi la Al Shabaab nchini Somalia na lile la kuuawa kwa wanafunzi takribani 148 wa Chuo Kikuu cha Garissa nchini Kenya yanadhihirisha namna ambavyo ugaidi ni hatari na tishio.

36. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inaungana na Jumuiya ya Kimataifa kulaani mauaji yanayofanywa na magaidi dhidi ya raia wasio na hatia.
37. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutumia fursa hii kuwasihi wazazi wenzangu wa Kitanzania kufuatilia kwa karibu mienendo ya watoto wao, kwani makundi ya kigaidi yana mtandao mpana wa kuwashawishi na kuwasajili vijana kwenye makundi hayo. Ndugu zangu Watanzania, tunapaswa kufahamu kwamba nchi yetu si kisiwa na hivyo hatuna budi kujiandaa na kuchukua tahadhari kutokana na changamoto za kiusalama zinazotokea kwa majirani zetu kwani jukumu la ulinzi wa nchi yetu ni letu sote na si la Serikali pekee. Aidha, nawashauri Watanzania wenzangu kujiepusha na chokochoko zinazoweza kuligawa Taifa na kuwaruhusu magaidi kupenyeza itikadi kali miongoni mwetu, na hivyo kuyapa makundi ya kigaidi mianya ya kuingia nchini na kufanya mashambulizi dhidi ya nchi yetu.

## UHUSIANO WA TANZANIA NA NCHI JIRANI

38. *Mheshimiwa Spika*, nchi yetu imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na majirani zetu ambapo ushirikiano wa shughuli za kiuchumi na kijamii unaimarika siku hadi siku. Ukiacha ziara zangu nilizotumwa kama Waziri wa Mambo ya Nje, ziara za juu kabisa za hivi karibuni za Mheshimiwa Rais Kikwete katika nchi jirani za Zambia, Burundi, Rwanda na Kenya na ziara za baadhi ya Viongozi Wakuu wa nchi hizo hapa nchini ni ishara tosha ya kuimarika kwa uhusiano huo. Aidha, mimi binafsi ninatarajia kufanya ziara ya kikazi nchini Rwanda baadaye mwaka huu.
39. *Mheshimiwa Spika*, uhusiano wa Tanzania na Kenya umeimarika ukiacha changamoto za hivi karibuni kuhusu magari ya kitalii ya Tanzania kushusha na kupakia watalii wanaotumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta; na suala la idadi ya safari za Shirika la Ndege la Kenya kuja Tanzania.

40. *Mheshimiwa Spika*, changamoto hiyo, ilianza kufanyiwa kazi baada ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya kutoa maelekezo ya muda mfupi kuwa mambo yarudi kama yalivyokuwa na kuelekeza Mawaziri wa Mambo ya Nje kusimamia mazungumzo ya pande mbili kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala hilo.
41. *Mheshimiwa Spika*, kama walivyoelekeza Waheshimiwa Marais, Mawaziri wa Sekta husika wa Tanzania walikutana na tayari wamekwisha wasilisha mapendekezo yao kwa Mheshimiwa Rais Kikwete. Hivi sasa, tunasubiri tarehe ya kukutana pamoja na wenzetu wa Kenya chini ya Uenyekiti wa Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania na Kenya.

### **Chaguzi za Nchi za Afrika na wajibu wa Watanzania kuelekea Uchaguzi Mkuu Oktoba 2015**

42. *Mheshimiwa Spika*, Bara la Afrika limeendelea kudhihirisha ukomavu wa demokrasia ambapo katika kipindi cha hivi karibuni baadhi ya nchi za Afrika zilifanya chaguzi zake na kufanikiwa kubadilisha viongozi wake kwa njia ya amani. Nchi hizo ni pamoja na Msumbiji, Botswana, Namibia, Mauritius, Zambia na Lesotho. Vilevile, nchi za Nigeria, Misri, Togo, Tunisia na Sudan. Kwenye chaguzi za Kusini mwa Afrika, Tanzania ilituma waangalizi kupitia mwamvuli wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).
43. *Mheshimiwa Spika*, licha ya changamoto zilizojitokeza, chaguzi hizo kwa kiasi kikubwa, zilifanyika katika hali ya utulivu, amani, uwazi, uhuru, haki, kuaminiana na kwa mujibu wa Sheria. Hiki ni kielelezo cha kuimarika kwa mifumo ya siasa, demokrasia na utawala bora kwenye ukanda wa SADC na Afrika kwa ujumla.

44. *Mheshimiwa Spika*, itakumbukwa kwamba, hadhi ya nchi inapimwa kwa namna watu wake wanavyoheshimu misingi ya demokrasia na haki za binadamu. Hivyo, uchaguzi ujao ni kipimo kingine cha ukomavu wetu kisiasa. Napenda kutumia fursa hii kuwatakia heri Watanzania wote katika uchaguzi huo.

## MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA MASUALA MUHIMU YA KIMATAIFA

### Sudan Kusini

45. *Mheshimiwa Spika*, mnamo mwezi Septemba 2014, Mheshimiwa Salva Kiir, Rais wa Jamhuri ya Sudan Kusini, kwa kutambua historia na uzoefu wa Tanzania katika kusuluhisha migogoro, alimuomba Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kupitia Chama chake kusaidia kutafuta suluhu ya kudumu ya mgogoro ndani ya chama cha “*Sudan People’s Liberation Movement (SPLM)*”.
46. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kukubali ombi hilo, Mheshimiwa Rais aliunda timu ndogo yenye uzoefu wa usuluhishi wa migogoro inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Samwel Malecela, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akisaidiwa na Katibu Mkuu wa CCM Ndugu Abdurahaman Kinana. Timu hiyo ilianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake tarehe 12 Oktoba, 2014 kwa kuyakutanisha makundi yanayohasimiana ya SPLM mjini Arusha, katika mazungumzo yanayojulikana kwa jina la *Arusha SPLM Intra-Party Dialogue*.
47. *Mheshimiwa Spika*, juhudi za upatanishi zimeanza kuzaa matunda ambapo tarehe 21 Oktoba, 2014 makundi matatu ya SPLM yanayohasimiana yalisaini makubaliano ya kukiunganisha tena chama hicho (*Agreement on the Reunification of the SPLM*) na kufuatiwa na Mwongozo wa Namna ya Kutekeleza Makubaliano

ya Kukiunganisha Chama hicho (*Road Map Agreement on SPLM Reunification*) tarehe 21 Januari, 2015. Mnamo mwezi Mei 2015, wadhamini wenza ambao ni CCM na *African National Congress* (ANC) walikutana Pretoria, Afrika Kusini kwa ajili ya kuweka mpango mkakati wa kurudi nyumbani Wanachama wa Zamani wa SPLM waliopo kizuizini. Ndugu Abdulrahman Kinana, Katibu Mkuu wa CCM alikutana na Mheshimiwa Cyril Ramaphosa, Naibu Rais wa Afrika Kusini, ambapo walikubaliana Wanachama hao waanze kurudi Juba, Sudan Kusini mwezi Juni 2015.

48. *Mheshimiwa Spika*, ni vyema ikafahamika kwa Bunge lako tukufu, Umma wa Watanzania pamoja na Dunia kwa Ujumla kuwa mchakato wa mazungumzo ya Arusha si mbadala wa mazungumzo ya amani ya IGAD yanayo endelea Addis Ababa bali yanalenga kusaidia kupatikana kwa amani ya kudumu nchini Sudan Kusini. Tunaamini kwamba, kuungana kwa makundi ya ndani ya SPLM kutarahisisha utatuzi wa mgogoro huo na kurejesha amani ya kudumu nchini humo.

### **Mpaka baina ya Tanzania na Malawi katika Ziwa Nyasa**

49. *Mheshimiwa Spika*, suala la mpaka baina ya Tanzania na Malawi kwenye Ziwa Nyasa bado lipo kwa msuluhishi na halijapatiwa ufumbuzi. Katika mkutano wa mwisho uliofanyika mwezi Machi 2014, pande zote mbili pamoja na msuluhishi zilikubaliana kuwa mchakato huo usogezwe mbele mpaka baada ya uchaguzi mkuu nchini Malawi uliofanyika Juni 2014. Mnamo mwezi Desemba 2014, Tanzania iliandika barua kwenda kwa Mheshimiwa Joachim Chisano, Rais Mstaafu wa Msumbiji na Mwenyekiti wa Jopo hilo kukumbusha kuhusu suluhu ya Mgogoro huo baada ya kupita takriban miezi sita bila kusikia chochote kutoka kwa msuluhishi.

50. *Mheshimiwa Spika*, Msimamo wa Tanzania bado ni uleule kwamba mpaka wetu na Malawi upo katikati ya ziwa na tumekubaliana kuwa suala hili limalizike kwa njia ya mazungumzo. Tumelifikisha suala hili mbele ya Jopo la Marais Wastaafu wa nchi za SADC na tumelipia ada yote inayotakiwa. Tunasubiri kuitwa.

## **Mgogoro wa Saharawi**

51. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania imeendelea kupinga vikali utawala wa mabavu wa Morocco katika nchi ya Saharawi. Tumeonyesha hayo wakati wa Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika Januari 2015 ambapo tuliunga mkono Azimio la kuzitaka Nchi Wanachama wa Umoja huo, Taasisi za kiraia za Afrika na taasisi nyingine za kimataifa kususia Mkutano wa Crans Montana, uliokuwa umepangwa kufanyika mwezi Machi 2015 kwa lengo la kuyatambua Mamlaka ya Morocco juu ya Saharawi.
52. *Mheshimiwa Spika*, licha ya mkutano huo kufanyika kama ulivyopangwa, nchi nyingi zilizoalikwa hazikushiriki. Aidha, Tanzania inaungana na Umoja wa Mataifa pamoja na Umoja wa Afrika katika kuunga mkono madai ya wananchi wa Saharawi ya kupewa haki ya kujiamulia mambo yao wenyewe kama nchi huru.
53. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inaendelea kuishauri Morocco kusikiliza sauti inayopazwa na watu wa Saharawi na Jumuiya ya Kimataifa ya kuipatia Saharawi fursa ya kupiga kura ya maoni (Referendum) ya kuamua iwapo wanataka wawe sehemu ya Ufalme wa Morocco au wanataka uhuru.



## **Mgogoro kati ya Palestina na Israel**

**54.** *Mheshimiwa Spika*, Jumuiya ya Kimataifa bado inaendelea na jitihada za kutafuta suluhu ya mgogoro huu wa muda mrefu. Tanzania inaunga mkono jitihada hizo, na kushauri pande husika kwenye mgogoro huo kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa mwaka 1967 kuhusu mgogoro huo. Makubaliano hayo ya mwaka 1967 yanatambua kuwepo kwa Taifa la Palestina na mpaka unaoeleweka. Tunasikitishwa na kauli za hivi karibuni za Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu za kutotambua uwepo wa Taifa la Palestina kinyume na msimamo wake wa siku za nyuma na viongozi wa Israel waliomtangulia. Tanzania inaamini kwamba suluhisho la kuwa na nchi mbili ambazo zitaishi kwa pamoja ikiwa ni Palestina huru na Israel salama ndio suluhisho la kudumu la mgogoro huo.

## **Mpango wa Nyuklia wa Iran**

**55.** *Mheshimiwa Spika*, Utawala wa Iran ulioingia madarakani mwaka 2013 ulifufua mazungumzo ya kutafuta suluhu ya Mpango wa Nyuklia wa Nchi hiyo na Mataifa matano Wanachama wa Kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Umoja wa Ulaya na Ujerumani. Mazungumzo hayo yaliyoanza Geneva, Uswisi tangu mwezi Februari 2014, yalisaidia kupatikana kwa makubaliano mapya kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Iran wa Matumizi Salama ya Nyuklia mnamo mwezi Aprili 2015.

**56.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inazipongeza pande zote mbili kwa kufikia hatua hiyo muhimu. Tunaamini hili ni somo kwa Jumuiya ya Kimataifa kuwa migogoro mingi inaweza kumalizwa kwenye meza ya mazungumzo. Tanzania inazitaka pande zote mbili kuongeza kasi ya kukamilisha majadiliano hayo.

## **Uhusiano kati ya Cuba na Marekani**

57. *Mheshimiwa Spika*, mwezi Desemba 2014, Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani na Kamaradi Raul Castro, Rais wa Cuba, walitoa matamko ya kuanza kurejesha uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi hizo. Uamuzi huo ulifuatiwa na utekelezaji wa makubaliano ya awali ikiwemo kubadilishana wafungwa wa kisiasa wa pande zote na vilevile, kwa Marekani kuiondoa Cuba katika orodha ya nchi zinazofadhili ugaidi duniani.
58. *Mheshimiwa Spika*, Rais Barack Obama atakumbukwa kwenye vitabu vya historia kama kiongozi aliyerejesha uhusiano mwema na Cuba na hivyo kufanya kuondolewa maazimio mbalimbali katika Umoja wa Mataifa yaliyolenga kuikandamiza Cuba. Tumempongeza Rais Obama na tunaendelea kuunga mkono msimamo wa Jumuiya ya Kimataifa wa kuitaka sasa Marekani kuiondolea Cuba vikwazo vya kiuchumi kwa manufaa ya watu wao. Tuna imani hilo nalo litafanyika.

## **Mgogoro wa Ukraine**

59. *Mheshimiwa Spika*, mgogoro wa Ukraine bado unaendelea, ingawa kuna jitihada za usuluhishi zinazofanywa na Jumuiya ya Kimataifa zikiongozwa na Umoja wa Ulaya (EU). Hatua iliyofikiwa hivi sasa ni ya kuridhisha na kutia matumaini. Kufuatia mazungumzo kati ya viongozi wa Urusi, Ukraine, Ujerumani na Ufaransa yaliyofanyika mjini Minsk, Belarus, mwezi Februari 2015 pande hizo zilifikia makubaliano ya kusimamisha mapambano kaskazini mwa Ukraine.
60. *Mheshimiwa Spika*, tangu kuanza kwa mgogoro huo, Tanzania tumeonyesha kutofungamana na upande wowote. Kutokana na siasa za undumilakuwili miongoni mwa Mataifa ya Magharibi, tumeendelea kufanya hivyo katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa hata pale lilipowasilishwa azimio kuhusu Ukraine (Azimio Na. A/68/L.39 lenye kichwa cha habari "*Territorial Integrity*

of Ukraine”) mwezi Machi 2014. Azimio hilo lilikuwa na maudhui makuu ya kuheshimu mamlaka, uhuru, umoja na mipaka ya Ukraine.

61. *Mheshimiwa Spika*, hata hivyo, Serikali ya Tanzania inaendelea kuunga mkono jitihada za Jumuiya ya Kimataifa kuhusu kurejesha hali ya amani na utulivu katika eneo hilo. Aidha, tunazishauri pande zinazohasimiana kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa kwa kuwa ndiyo njia muafaka ya kutatua mgogoro huo bila kusababisha maafa zaidi kwa binadamu.

## MAFANIKIO YA WIZARA KWA KIPINDI CHA AWAMU YA NNE

62. *Mheshimiwa Spika*, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya mwisho nikiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wa Serikali ya Awamu ya Nne, nafurahi kuelezea kwa kifupi baadhi ya mafanikio ambayo Wizara inajivunia kwa kipindi cha Awamu hii kama ifuatavyo:-

- (i) Tumefungua Balozi mpya katika nchi za Malaysia, Brazil, Comoro, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu na Kuwait. Aidha, tumefanikiwa kufungua upya Ubalozi wa Tanzania The Hague, Uholanzi uliofungwa mwaka 1994. Kadhalika, Balozi mpya za Brazil, Oman, Uturuki, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na Namibia zilifunguliwa hapa nchini katika kipindi hicho. Kwa sasa tuna jumla ya Balozi 35 nje ya nchi na ni wenyeji wa Balozi 62 pamoja na Mashirika ya Kimataifa 23 hapa nchini;
- (ii) Tumenunua majengo kwa ajili ya Ofisi na Makazi ya watumishi katika Balozi za Tanzania katika miji ya New York na Paris. Aidha, tumeyafanyia ukarabati mkubwa majengo yetu yaliyopo Maputo, Msumbiji;
- (iii) Tanzania imepewa heshima kubwa kuwa mwenyeji wa Taasisi mbalimbali za Kimataifa. Baadhi ya Taasisi hizo ni Mahakama ya Afrika

ya Haki za Binadamu na Watu; Bodi ya Ushauri ya Umoja wa Afrika ya kupambana na Rushwa (*AU Advisory Board on Corruption*); Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa (*African Institute on Interanational Law*); Mahakama Maalum itakayorithi majukumu pamoja na kutunza Kumbukumbu za Kesi za iliyokuwa ICTR (*The United Nations Merchanism for International Criminal Tribunals-UNMICT*);

- (iv) Tumepata ardhi katika eneo la Lakilaki Mkoani Arusha, ambapo Mashirika yenye Hadhi ya Kidiplomasia yatajenga Ofisi za kudumu. Tayari UN-MICT imekamilisha taratibu zote za kuanza ujenzi huku upande wa Tanzania unakamilisha jukumu lake la kusogeza miundombinu muhimu kwenye eneo hilo;
- (v) Mwaka 2008, Tanzania ilitoa mchango mkubwa katika kumaliza mgogoro ulioikumba Comoro kufuatia Kanali Mohamed Bacar, Kiongozi wa Kisiwa cha Anjouan kuasi na kung'ang'ania madaraka baada ya kumaliza muhula wake wa uongozi. Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) liliongoza juhudi za kumng'oa muasi huyo kwa kushirikiana na majeshi kutoka Sudan na Libya pamoja na Senegal na hivyo kurejesha utawala wa kikatiba nchini Comoro;
- (vi) Vilevile, Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya za Kikanda imefanikiwa si tu kutatua migogoro ya kisiasa katika nchi za Madagascar, Burundi, DRC, Cote d'Voire, Zimbabwe na hivi karibuni Sudan Kusini, bali pia kuchangia katika vikosi vya kulinda amani duniani. Kadhalika, kutokana na mchango wetu na nidhamu ya jeshi letu, Watanzania wawili wameteuliwa kuongoza Kamandi za kulinda amani. Luteni Jenerali Paul Ignas Meela anaongoza UNAMID nchini Sudan na Brigedia Jenerali Ramadhani Kimweri ambaye ni Kamanda wa FIB ya MONUSCO nchini DRC. Tanzania inaamini kuwa bila majirani salama hakuna mafanikio ya kiuchumi;
- (vii) Tumefanikisha Watanzania kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali kwenye vyombo vya Kimataifa. Baadhi ya Watanzania hao ni Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; Balozi Amina Salum Ali, Mwakilishi

wa Kudumu wa Umoja wa Afrika nchini Marekani; Mhe. Prof. Anna Tibaijuka, Katibu Mtendaji wa Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (UN-HABITANT); Dkt. Winnie Mapunju Shumbusho, Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Afya Duniani (WHO); Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa SADC; Balozi Liberata Mulamula, aliyekuwa Katibu Mtendaji wa Kwanza wa Jumuiya ya Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR); Jaji Agustino Ramadhani, Rais wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; Balozi James Kateka, Jaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria za Bahari; Profesa Chris Peter Maina, Mjumbe kwenye Kamisheni ya Sheria ya Umoja wa Mataifa; Balozi Augustine Mahiga, aliyekuwa Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu mgogoro wa Somalia, Brigadia Jenerali Sara T. Lwambali, Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Afrika, Juba - Sudan Kusini na Balozi Wilfred Ngirwa, Mwenyekiti wa Baraza la Shirika la Chakula Ulimwenguni (FAO). Aidha, hivi karibuni Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Watu Mashuhuri kwenye Tume Huru ya Masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa;

- (viii) Tumepokea viongozi mashuhuri kutoka nchi mbalimbali kwenye ukanda wa Afrika na nje ya Afrika. Ziara hizo ni kiashiria cha kuimarika kwa uhusiano wa kidiplomasia baina ya nchi yetu na nchi hizo na kuongeza kasi ya kuvutia uwekezaji na kutangaza utalii;
- (ix) Wizara ilitunukiwa Tuzo kutoka Umoja wa Watendaji Wakuu wa Sekta Binafsi (*CEO Round Table*) hapa nchini kwa kutambua mchango wa Wizara yangu katika kukuza sekta binafsi nchini;
- (x) Tumeanzisha Idara kamili ya Diaspora kufuatia kutambua umuhimu wa kuwahusisha Watanzania waishio Ughaibuni katika kuchangia maendeleo ya nchi;
- (xi) Tumejenga ukumbi wa kisasa wa Mikutano wenye hadhi ya Kimataifa wa Julius Nyerere kwa lengo la kukuza utalii wa mikutano;

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

63. *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali na Sekta Binafsi imeendelea kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo. Pamoja na mambo mengine, majukumu hayo yametekelezwa kupitia: ushiriki wetu katika mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa; ziara za Viongozi wa Kitaifa nje ya Nchi; ziara za Viongozi wa Kitaifa wa mataifa mengine hapa Nchini; na Ofisi zetu za uwakilishi nje ya nchi. Naomba kutumia fursa hii, kuainisha namna majukumu hayo yalivyotekelezwa.

### USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

64. *Mheshimiwa Spika*, napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha Mwaka wa Fedha, 2014/15 Tanzania imeendelea kuwa mwanachama mwaminifu katika Jumuiya ya Kimataifa na kushiriki kikamilifu kwenye mikutano mbalimbali ya jumuiya hizo. Wizara yangu imefanikiwa kuratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mikutano hiyo ya Kimataifa kama nitakavyoeleza katika aya zinazofuata.

### Kikao cha 69 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA)

65. *Mheshimiwa Spika*, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliongoza ushiriki wa Tanzania katika kikao cha 69 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilichofanyika New York, Marekani kuanzia mwezi Septemba hadi Desemba 2014, chini ya kaulimbiu “*Delivering on and Implementing a Transformative Post-2015 Development Agenda*”. Kaulimbiu hii inabainisha azma ya Jumuiya ya Kimataifa ya kuendesha majadiliano yatakayohitimishwa kwa kupitishwa kwa ajenda mpya ya maendeleo

itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka 15 ijayo kuanzia Januari 2016. Utekelezaji wa ajenda mpya ya maendeleo utaanza baada ya kuhitimishwa kwa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo ya Milenia mwishoni mwa mwaka 2015.

66. *Mheshimiwa Spika*, akihutubia Mkutano huo, Mheshimiwa Rais, pamoja na mambo mengine, alieleza Jumuiya ya Kimataifa msimamo wa Tanzania katika masuala mbalimbali yakiwemo usalama, afya, hususan ugonjwa wa Ebola, utekelezaji wa Malengo ya Milenia na mchakato wa kupata Ajenda Mpya ya Maendeleo baada ya mwaka 2015.

### **Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs) na Ajenda ya Maendeleo baada ya Mwaka 2015 (P2015DA)**

67. *Mheshimiwa Spika*, dunia inajiandaa kuanza kutekeleza Ajenda mpya ya Maendeleo (*Post 2015 Development Agenda*) ifikapo mwezi Januari 2016, kufuatia kipindi cha utekelezaji wa Malengo ya Milenia (MDGs) kumalizika mwezi Desemba 2015. Agenda hiyo itakuwa na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Tanzania ilituliwa kuwa miongoni mwa nchi 30 zilizounda Kikundi Kazi cha kuandaa Malengo ya Maendeleo Endelevu. Malengo ya Maendeleo Endelevu 17 na shabaha zake 169 zilipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 2014.

68. *Mheshimiwa Spika*, msimamo wa Tanzania kwenye majadiliano hayo ni kwamba Ajenda Mpya ilenge kukamilisha utekelezaji wa Malengo ya Milenia ambayo hayajakamilika; kuwapo kwa vyanzo vya rasilimali za kutekeleza ajenda mpya; kuwekwa mfumo wa ufuatiliaji; na kwamba ajenda hiyo kamwe isitumiwe na Mataifa makubwa kupitisha kwa kificho ajenda ambazo zinapingana na mila, tamaduni, desturi na imani zetu kwa kisingizio cha usawa na haki za binadamu.

## Mkutano wa Mabadiliko ya Tabianchi

- 69.** *Mheshimiwa Spika*, suala la Mabadiliko ya Tabianchi ni tishio kubwa kwa ukuaji na ustawi wa dunia nzima. Tumeshuhudia kuongezeka kwa ukame, mafuriko, vimbunga, magonjwa na kupotea kwa baadhi ya wanyama na mimea ni ishara ya madhara makubwa ya mabadiliko ya tabianchi. Kufuatia hali hiyo, ushiriki wa Tanzania kwenye Mikutano ya Mabadiliko ya Tabianchi umeimarishwa.
- 70.** *Mheshimiwa Spika*, Mikutano wa 20 wa Mabadiliko ya Tabianchi na Mikutano wa 10 wa Itifaki ya Kyoto ulifanyika Lima, Peru mwezi Desemba 2014. Mikutano huo uliazimia kuanzisha Mkataba mpya wa Mabadiliko ya Tabianchi utaochukua nafasi ya Itifaki ya Kyoto. Mkataba huo wa Mabadiliko ya Tabianchi utakubaliwa rasmi Desemba 2015 mjini Paris, Ufaransa.
- 71.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mara ya kwanza, Marekani na China ambao si wanachama wa Mkataba wa Kyoto zilionesha azma ya kujiunga na Mkataba Mpya. Aidha, nchi hizo zimeahidi kuchangia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (*Green Climate Change Fund*). Fedha hizo zitatumika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi kwenye nchi zinazoendelea. Nchi yetu inakaribisha hatua hiyo ya Mataifa makubwa kujiunga katika jitihada za mapambano dhidi ya Mabadiliko ya Tabianchi. Tanzania inazitaka nchi zote duniani kujiunga na Mkataba huo mpya wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, nchi zile zinazochafua zaidi mazingira zione zina wajibu wa kuchangia zaidi katika kukabiliana na maafa ya Mabadiliko ya Tabianchi.



## **Mkutano wa Kimataifa kuhusu Biashara Haramu ya Wanyamapori**

- 72.** *Mheshimiwa Spika*, kushamiri kwa biashara haramu ya wanyamapori katika miaka ya hivi karibuni kumeathiri jamii, uchumi, mazingira na usalama wa nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania. Kwa kulitambua hilo, mwezi Machi 2015 katika mji mdogo wa Kasane, Botswana ulifanyika mkutano wa pili wa Kimataifa kuhusu Biashara Haramu ya Wanyamapori (*Kasane Conference on Illegal Trade in Wildlife*). Lengo la Mkutano huo lilikuwa ni kupitia hatua za utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa na Jumuiya ya Kimataifa wakati wa mkutano kama huo uliofanyika London, Uingereza mwezi Februari 2014. Aidha, mkutano huo ulitoa fursa kwa nchi washiriki kubadilishana uzoefu wa namna ya kukabiliana na tatizo hili sugu.
- 73.** *Mheshimiwa Spika*, Ujumbe wa Tanzania kwenye Mkutano huo uliongozwa na Dkt. Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliifahamisha Jumuiya ya Kimataifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kupambana na ujangili wa wanyamapori. Aidha, alieleza umuhimu wa kudumisha ushirikiano kati ya nchi na nchi ikiwa ni pamoja na kushirikiana na nchi zenye uhitaji mkubwa wa bidhaa za wanyamapori ili kutokomeza kabisa soko hilo haramu.
- 74.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na masuala mengine, Mkutano huo pia uliazimia kuongeza ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kupunguza mahitaji na ununuzi wa bidhaa haramu za wanyamapori; kuwezesha ufanisi wa vyombo vinavyosimamia sheria kwa kuvipatia rasilimali, ujuzi na uwezo wa kuchunguza na kushitaki uhalifu dhidi ya wanyamapori; na kuandaa rasimu ya azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu ujangili na usafirishaji wa bidhaa haramu za wanyamapori.

## ULINZI NA UJENZI WA AMANI DUNIANI

75. *Mbeshimiwa Spika*, Tanzania imeendelea kuchangia vikosi vya kulinda amani katika maeneo mbalimbali duniani. Kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa, hadi kufikia mwezi Februari 2015, Tanzania inashika nafasi ya kumi na tatu (13) miongoni mwa nchi mia moja na ishirini (120) zinazochangia askari katika operesheni za kulinda amani duniani. Kwa sasa, Tanzania inachangia askari katika vikosi vya kulinda amani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (MONUSCO), katika jimbo la Abyei (UNISFA), na jimbo la Darfur (UNAMID) nchini Sudan, Lebanon (UNIFIL), Ivory Coast (UNOCI) na Sudan Kusini (UNMISS).
76. *Mbeshimiwa Spika*, ushiriki wetu kwenye Operesheni hizo, pamoja na kuwa ni mchango wetu kwa dunia katika kuendeleza amani na kuwalinda wananchi wasiokuwa na hatia dhidi ya athari za mapigano, pia unatoa fursa kwa vikosi vyetu kupata uzoefu, maarifa, weledi na kujifunza mbinu mpya zinazohusiana na ulinzi wa amani.
77. *Mbeshimiwa Spika*, Wizara kupitia Uwakilishi wetu wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa, na kwa kushirikiana na mataifa mengine yanayochangia vikosi vya kulinda amani, inaendelea na majadiliano ya kuutaka Umoja wa Mataifa kuangalia upya viwango vya malipo vinavyotolewa kwa vikosi hivyo pamoja na malipo ya vifaa na zana zinazotumika katika kazi hiyo.

## USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA UMOJA WA AFRIKA NA JUMUIYA ZA KIKANDA

### Umoja wa Afrika

78. *Mbeshimiwa Spika*, katika maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika/OAU, Nchi Wanachama ziliazimia kuanzisha dira na mpango kazi wa miaka 50 ujulikanao kama Ajenda 2063. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwenye Mkutano wa 24 wa Umoja wa Afrika uliofanyika Mwezi Januari, 2015 mjini Addis Ababa, Ethiopia Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja huo walipitisha Ajenda 2063 ambayo ni Dira ya miaka 50 ijayo ya Bara la Afrika. Dira hiyo inazitaka Nchi Wanachama kufanya kazi kwa lengo la kujenga Afrika salama yenye umoja na kujitegemea bila kuathiri maadili ya Kiafrika.
79. *Mbeshimiwa Spika*, pamoja na mambo mengine, Dira hii imelenga kuimarisha umoja na mshikamano kwa Nchi za Afrika huku ikisisitiza kuhusu kuondoa umaskini, kuboresha elimu, kulinda amani, kuendeleza viwanda na kilimo, kutunza mazingira na kuunganisha Bara la Afrika kwa miundombinu ya kisasa. Aidha, mpango wa miradi inayopewa kipaumbele unatarajiwa kujadiliwa na kupitishwa mwishoni mwa mwezi Juni 2015 wakati wa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika utakaofanyika Pretoria, Afrika Kusini.
80. *Mbeshimiwa Spika*, ili kufanikisha utekelezaji wa Dira hiyo, Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika zinatakiwa kuingiza Malengo ya Ajenda 2063 kwenye Mipango yao ya Maendeleo. Kwa Tanzania tunatakiwa kuingiza Ajenda hiyo kwenye Mipango yetu ya Maendeleo iliyopo na itakayobuniwa, ili isikinzane katika utekelezaji wake.

## **Uenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (*Committee of African Heads of State and Government on Climate Change-CAHOSCC*)**

- 81.** *Mheshimiwa Spika*, wakati wa mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, Mheshimiwa Rais Kikwete alimaliza muda wake kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (CAHOSCC).
- 82.** *Mheshimiwa Spika*, wakati akikabidhi Uenyekiti wa CAHOSCC kwa Mheshimiwa Abdel Fattah el-Sisi, Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri, Mheshimiwa Rais alisisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuendelea kuzungumza kwa sauti moja katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kutoa kipaumbele kwenye masuala ya upatikanaji wa fedha, teknolojia, na kuijengea Afrika uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.
- 83.** *Mheshimiwa Spika*, mafanikio makubwa yaliyotokana na Uenyekiti wa Mheshimiwa Rais kwenye CAHOSCC ni kuweza kusimamia na kuendeleza mikakati yenye kutetea ajenda ya Afrika kuhusu mabadiliko ya Tabianchi pamoja na kuongoza ushiriki wa Afrika kwenye Mkutano wa Ngazi ya Juu ulioandaliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Septemba 2014.

## **Umoja wa Afrika Kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere**

- 84.** *Mheshimiwa Spika*, sanjari na Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari 2015 viongozi hao waliamua kwa kauli moja kulipa Jengo jipya la Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika jina la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Wakuu hao wa Nchi na Serikali walifikia uamuzi huo si tu kwa kutambua na

kuenzi mchango wa Baba wa Taifa na nchi yetu katika harakati za ukombozi na kupigania Uhuru, bali pia jitihada za Tanzania katika kutatua migogoro Barani Afrika. Uamuzi huo unatoa fursa ya kuitangaza nchi yetu kimataifa na pia kuwezesha vizazi vijavyo kuendelea kutambua na kuenzi mchango huo katika harakati za ukombozi na utatuzi wa migogoro Barani Afrika.

## **Watanzania kushika nyadhifa mbalimbali katika Taasisi za Umoja wa Afrika**

- 85.** *Mheshimiwa Spika*, ninayo furaha ya kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, wakati wa Mkutano wa 24 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, mwezi Januari 2015, Watanzania wawili walichaguliwa kushika nyadhifa katika Taasisi za Umoja huo.
  
- 86.** *Mheshimiwa Spika*, Prof. Tolly S. Mbwete alichaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Chuo cha Afrika (*Pan-African University Council*) na Bw. Ekwabi Mujungu, alichaguliwa kuwa miongoni mwa wajumbe kumi na mmoja (11) wa Bodi ya Ushauri wa Kupambana na Rushwa ya Umoja wa Afrika (AUABC) kwa kipindi cha miaka miwili (2). Kuchaguliwa kwa Watanzania hao ni ishara ya kuendelea kuaminika kwa nchi yetu kwenye medani za kimataifa.

## **Nafasi ya Tanzania katika Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika**

- 87.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia 2014 hadi 2016 Tanzania inakua Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika. Kupitia Baraza hilo, Tanzania imeendelea kutoa mchango mkubwa katika harakati za kutafuta amani Barani Afrika, ikiwemo Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Somalia na Sudan.

88. *Mheshimiwa Spika*, aidha, kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Ebola kwenye nchi za Afrika Magharibi, Tanzania iliitikia wito wa Baraza hilo wa kupeleka Kikosi Maalum cha Umoja wa Afrika kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huo kwa kuchangia wataalam wa afya. Operesheni hiyo inayoendelea hadi mwezi Juni 2015 imefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Naomba kutumia fursa hii, kuwapongeza wataalam hao ambao ni Ndg. Justin Maeda, Dkt. Ferilinda Temba, Ndg. Saasita Shaban, Ndg. Godbless Lucas na Ndg. Theophil Malibiche, kwa kujitolea kwenda kusaidia Waafrika wenzetu katika wakati mgumu na hatari wa gonjwa la Ebola. Huu ni mfano wa kishujaa unaofaa kuigwa.

### **Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa AU wa mwaka 2017**

89. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania kwa mara ya kwanza inatarajiwa kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika unaotarajiwa kufanyika mwaka 2017. Umuzi huo ulifikiwa baada ya Tanzania kuwasilisha maombi yake katika vikao vya umoja huo mwaka 2012 na kukubaliwa.

90. *Mheshimiwa Spika*, Mkutano huo ni heshima kubwa kwa nchi yetu na utatoa fursa kwa Watanzania kuongeza kipato kutokana na biashara ya huduma. Aidha, kufanyika kwa mkutano huo nchini kutatoa fursa ya kutangaza utalii pamoja na diplomasia ya mikutano.

Hivyo, ni vyema ndugu zangu wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla tukajiandaa vilivyo ili kuhakikisha kwamba tunanufaika na fursa zitakazotokana na mkutano huo.

### **Jumuiya ya Afrika Mashariki**

91. *Mheshimiwa Spika*, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, katika Mkutano wa Kumi na Sita wa Viongozi Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika

Mashariki uliofanyika tarehe 20 Februari, 2015 jijini Nairobi, Kenya, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichukua nafasi ya Uenyekiti wa Jumuiya hiyo.

92. *Mheshimiwa Spika*, Mheshimiwa Rais ameelekeza kuwa, wakati wa Uenyekiti wa Tanzania, vipaumbele vitakuwa: kurasimisha biashara zisizo rasmi ili ziweze kuchangia mapato katika Serikali za nchi wanachama na kuchangia katika upatikanaji wa takwimu muhimu za kibiashara; kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kodi (Non Tariff Barriers); kuongeza mapato kwa ajili ya ufadhili wa ujenzi wa miundombinu ili iendane na kasi ya mtangamano; na kuongeza kasi ya majadiliano ya mchakato wa kupata viashiria vya kiuchumi ambavyo ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika hatua ya ushirikiano wa Umoja wa Fedha. Ni matumaini yetu kwamba kila nchi itatimiza wajibu wake ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele hivi tukiwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

### **Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)**

93. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania imeendelea kushiriki kikamilifu katika mikutano ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Mjadala mkubwa kwa sasa ni Mkakati wa Uendeshaji Viwanda wa SADC ambao ndiyo Nguzo ya Kwanza ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya SADC kwa mwaka 2015-2020 (*SADC Regional Indicative Strategic Development Plan – RISDP 2015-2020*).
94. *Mheshimiwa Spika*, Mkakati huu unaenda sambamba na utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na ule wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ambao viwanda ni moja ya Sekta ya vipaumbele. Wizara yangu inawasihi wafanyabiashara kujipanga ili kuweza kunufaika na fursa hii.

## **Jumuiya ya Nchi zilizo katika Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR)**

95. *Mheshimiwa Spika*, Jumuiya ya Nchi zilizo katika eneo la Maziwa Makuu (ICGLR) imeendelea kukabiliana na changamoto ya hali ya ulinzi na usalama katika Jumuiya hiyo ambayo imekuwa ikibadilika mara kwa mara kutokana na hali ya machafuko iliyopo katika eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Tanzania itaendelea kuunga mkono juhudi za ICGLR katika kutafuta amani ya kudumu katika ukanda wa Maziwa Makuu.

## **Jumuiya ya Nchi zilizo katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA)**

96. *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inanufaika na uanachama wake wa Jumuiya ya Nchi zilizo katika mwambao wa Bahari ya Hindi (IORA). Wizara imeendelea kuwa kiungo muhimu kati ya nchi yetu na Jumuiya hiyo kwenye masuala ya maendeleo kwa kuratibu ushiriki wa wataalam katika mikutano inayoratibiwa na Jumuiya hii yenye lengo la kujenga uwezo katika nyanja za uchumi, biashara, uvuvi, utalii na fedha.

## **Maandalizi ya uzinduzi wa Eneo Huru la Biashara la Utatu wa COMESA - EAC - SADC (COMESA - EAC - SADC Tripartite Free Trade Area)**

97. *Mheshimiwa Spika*, katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Kanda za COMESA, EAC na SADC walipokutana Kampala mwezi Oktoba 2008, Mheshimiwa Jakaya Mrisho kikwete, alitumia ushawishi wake mkubwa kufanikisha makubaliano ya kuanza majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu huo wa COMESA, EAC na SADC.
98. *Mheshimiwa Spika*, eneo hilo la utatu linalojumuisha nchi 26 na idadi ya watu wapatao milioni 527 sawa na asilimia 57 ya watu wote Barani Afrika,



linakadiriwa kuwa na Pato la Taifa (GDP) la Dola za Marekani bilioni 624.

99. *Mheshimiwa Spika*, wakati majadiliano hayo yanaendelea, naendelea kutoa wito na kuwakumbusha wafanyabiashara wa Tanzania kujiandaa vizuri ili kuiwezesha nchi kunufaika na fursa hiyo.

## **KUSIMAMIA MIKATABA NA MAKUBALIANO YA KIMATAIFA**

100. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza jukumu la kusimamia Mikataba na Makubaliano baina ya Tanzania, nchi nyingine na Taasisi za Kimataifa, Wizara yangu inaendelea kuratibu na kusimamia uwekwaji saini wa Mikataba hiyo. Katika mwaka huu wa fedha tumeratibu kusainiwa kwa mikataba ifuatayo:-

- (i) Mkataba wa Kukuza, Kutangaza na Kulinda Uwekezaji baina ya Tanzania na Jamhuri ya Kiislam ya Iran;
- (ii) Makubaliano baina ya Chuo cha Diplomasia Tanzania na Taasisi ya Mambo ya Nje ya Argentina;
- (iii) Mkataba baina ya Tanzania na Vietnam kuhusu usafiri wa Majini;
- (iv) Makubaliano (MOU) baina ya Wizara ya Uchukuzi ya Tanzania na Wizara ya Biashara ya China kuhusu masuala ya Usafiri wa Anga;
- (v) Makubaliano (MOU) baina ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania na Wizara ya Usimamizi wa Misitu ya China kuhusu Uhifadhi wa Wanyamapori na Maliasili; na
- (vi) Makubaliano ya Awali baina ya Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) na Mfuko wa China wa Maendeleo ya Afrika.

**101.** *Mheshimiwa Spika*, mwezi Novemba 2014, Wizara yangu iliitikia wito wa Bunge lako kutoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu Mikataba ya Kimataifa na mchakato wa Tanzania kuridhia mikataba hiyo. Semina hiyo ilikuwa ya mafanikio na Wizara iko tayari kushirikiana na Bunge lako kuendelea kutoa semina za masuala ya mikataba na sheria mbalimbali za kimataifa kwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

## **WATANZANIA WAISHIO UGHAIBUNI (DIASPORA)**

**102.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kuwatambua na kuwahamasisha Watanzania waishio ughaibuni kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi. Tumekuwa tukishirikiana na Watanzania hao kuimarisha Jumuiya zao na kuanzisha nyingine kwenye maeneo ambayo hazikuwepo awali kama vile Comoro, Urusi, na Namibia.

**103.** *Mheshimiwa Spika*, ushirikiano huo umewezesha kujenga imani ya Wanadiaspora kwa Serikali yao na hivyo kujenga hamasa ya kushiriki katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania waishio ughaibuni ambao bado hawajajisajili kwenye Jumuiya za Watanzania, kufanya hivyo ili kurahisisha upatikanaji wa takwimu zao.

**104.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na *Tanzania Diaspora Initiative* (TDI), iliandaa na kufanikisha kongamano la kwanza la *Diaspora (Diaspora Home Coming Conference)* lililofanyika Dar es salaam mwezi Agosti 2014. Kongamano hilo lililofunguliwa na Mheshimiwa Rais na Kufungwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lilifanyika kwa mafanikio makubwa ambapo W anadiaspora wa Tanzania kutoka nchi 23 duniani, pamoja na Watanzania waliowahi kuishi na kufanya kazi ughaibuni walihudhuria.

- 105.** *Mheshimiwa Spika*, kongamano hilo liliwakutanisha wanadiaspora wa Tanzania, Wizara na Taasisi nyingine za Umma pamoja na sekta binafsi ili kujadili namna bora ya ushirikishwaji wao katika maendeleo ya nchi. Kongamano jingine kama hilo linatarajiwa kufanyika mwezi Agosti mwaka huu kwa lengo la kupata mrejesho wa yatokanayo na Kongamano la kwanza na kupanga mikakati mipya.
- 106.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia masuala ya Uhamiaji (IOM), Mwezi Aprili 2015, Wizara ilizindua *Tanzania Migration Profile* ambayo ina taarifa muhimu za Watanzania waishio ughaibuni ikiwa ni pamoja na viwango vyao vya elimu, ujuzi na shughuli wanazofanya.
- 107.** *Mheshimiwa Spika*, aidha, Wizara imekamilisha *Diaspora web-portal* ambayo itarahisisha mawasiliano na kuharakisha upashanaji habari baina ya Jumuiya za Watanzania waishio ughaibuni na Wizara. Mbali na kurahisisha mawasiliano, *portal* hiyo pia inataarifa mbalimbali za nyumbani, shughuli za Serikali zinazowahusu pamoja na taarifa za fursa ambazo Watanzania hao wanaweza kuzitumia kama njia yao ya kuchangia maendeleo nyumbani na wao kuleta fursa mbalimbali zinazopatikana ughaibuni.
- 108.** *Mheshimiwa Spika*, Wanadiaspora wamekuwa wakiomba kuandikishwa na kupewa vitambulisho vya Taifa pamoja na haki ya kupiga kura wakiwa ughaibuni. Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) tumefanikiwa kuweka utaratibu maalum ili Wanadiaspora waweze kujiandikisha na kupewa vitambulisho hivyo wanapotembelea nyumbani. Tunaendelea kufanya mazungumzo na mamlaka husika ili Balozi zetu ziweze kuwaandikisha Watanzania hao na hatimaye kupata vitambulisho hivyo.

**109.** *Mheshimiwa Spika*, ninatambua kuwa sheria na mazingira ya sasa hayaruhusu Balozi zetu kuratibu upigaji wa kura kwa Wanadiaspora, lakini natoa rai kwa wadau wa masuala ya chaguzi hapa nchini waendeleo kushauri namna bora ya kuwashirikisha Watanzania wenzetu kwenye maamuzi makubwa ya nchi yetu ikiwemo upigaji kura kwa ngazi ya Rais kama ambavyo baadhi ya nchi wameweza kufanikisha hilo.

## **MASUALA YA DIPLOMASIA, ITIFAKI, UWAKILISHI NA HUDUMA ZA KIKONSELI**

### **Diplomasia**

**110.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu imeendelea kuimarisha diplomasia ya Tanzania. Jukumu hili tumekuwa tukilitekeleza kupitia ziara mbalimbali pamoja na kuanzisha uhusiano na nchi nyingine rafiki. Mathalan, mwezi Januari 2015 nilifanya ziara ya kikazi nchini Urusi kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Sergey Lavrov, Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi. Lengo kuu la ziara hiyo lilikuwa ni kuimarisha uhusiano uliopo baina ya nchi zetu. Kadhalika, tulitumia fursa hiyo kujadiliana namna ya kuendeleza ushirikiano ikiwemo kuanzisha Tume ya Kudumu ya Ushirikiano ya Pamoja ambayo itatilia mkazo kukuza biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Urusi. Baadhi ya kampuni za nchi hiyo zikiwemo Gazprom, Lukoil na Rosatom tayari zimeonesha nia ya kuwekeza nchini.

**111.** *Mheshimiwa Spika*, vilevile, mwezi Mei 2015, Mheshimiwa Rais Kikwete alifanya ziara ya kikazi nchini Algeria kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Abdelaziz Bouteflika, Rais wa nchi hiyo. Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Rais Kikwete alipata fursa ya kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, kutembelea Kampuni ya Mabasi na Malori ya Algeria na pia kukutana na wanafunzi wa Kitanzania wanaosoma nchini humo.

- 112.** *Mheshimiwa Spika*, wakati Tanzania na Algeria zikikubaliana kuendeleza ushirikiano katika sekta mbalimbali hususan elimu, kampuni za nishati za Algeria zimeonyesha nia ya kuwekeza katika sekta ya nishati nchini. Aidha, Mheshimiwa Rais Kikwete aliahidi kufungua Ubalozzi nchini humo kwa ajili ya kuendeleza ushirikiano kati ya nchi hizi mbili pamoja na kutoa huduma za kikonseli kwa Watanzania waliopo Algeria.
- 113.** *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyodokeza hapo awali, tumeendelea kupokea maombi kutoka nchi mbalimbali duniani ya kuanzisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi yetu. Miongoni mwa nchi tulizopokea maombi hayo ni pamoja na: Moldova, Fiji, Solomon Islands, Azerbaijan, Paraguay, Bosnia and Herzegovina, Saint Vincent and The Grenadines, Georgia, Kyrgyzstan, Marshall Islands, Latvia, Ecuador, Malta, Kosovo, Montenegro, na Kazakhstan. Hivi sasa tupo mbioni kukamilisha mikataba ya kuingia katika uhusiano huo.

## **Huduma za Itifaki na Uwakilishi**

- 114.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu inaendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa jukumu la kutoa huduma za itifaki na uwakilishi. Katika kutekeleza hilo, tumewezesha upatikanaji wa viza kwa Viongozi na Watumishi wa Serikali wanaosafiri kikazi katika nchi mbalimbali. Wizara inawakumbusha Viongozi na Watendaji wote wenye hati za kidiplomasia wanaotumia huduma za Wizara katika kuomba viza za nchi mbalimbali kuwasilisha maombi yao mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.
- 115.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande mwingine tumeendelea kurahisisha upatikanaji wa viza kwa wageni wanaotaka kutembelea nchi yetu kwa sababu mbalimbali hususan utalii, kutafuta fursa za uwekezaji, michezo na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Kimataifa.

- 116.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara inatambua changamoto wanazozipata Watanzania katika upatikanaji wa viza katika nchi mbalimbali. Kutokana na hilo, Wizara inaendelea kuzishawishi nchi hizo kurahisisha upatikanaji wa viza na kufungua na kurudisha Ofisi za kutolea viza hapa nchini.
- 117.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuchukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali ya Canada imerudisha utaratibu wa kutoa viza hapa nchini. Kabla ya uamuzi huo awali viza za Canada zilikuwa zikitolewa nchini Kenya. Tunaamini kuwa, uamuzi huo utasaidia kupunguza usumbufu wa upatikanaji wa viza kwa wananchi pamoja na viongozi wa Serikali. Aidha, tunaziomba nchi zingine ambazo hazina utaratibu wa kutoa viza hapa nchini zione umuhimu wa kurejesha huduma hiyo.

### **Huduma za Kikonseli**

- 118.** *Mheshimiwa Spika*, katika kukabiliiana na machafuko yanayoendelea duniani, Wizara yangu imekuwa ikiratibu juhudi za Serikali kuwarudisha Watanzania wanaojikuta katikati ya hali ya mapigano, vita au gharika (*Natural Calamities*). Hadi kufikia mwezi Mei 2015, tumefanikisha kuwarejesha nchini Watanzania wapatao 62 kutoka nchini Yemen.

### **MASHAMBULIZI YA WAGENI NCHINI AFRIKA KUSINI**

- 119.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia mashambulizi ya Wenyeji dhidi ya Wageni yaliyozuka mwezi Aprili, 2015 nchini Afrika Kusini, Tanzania ilichukua hatua za makusudi za kuwarejesha nyumbani Watanzania wapatao 26. Tanzania inalaani vikali vitendo hivyo vya kibaguzi na visivyo vya kiungwana, vilivyofanywa na baadhi ya wananchi wa Afrika Kusini dhidi ya wageni.

**120.** *Mheshimiwa Spika*, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa Watanzania wanaoishi kwenye nchi zenye machafuko wanarejea nyumbani salama. Lakini naomba nitoe rai kwa Watanzania wanaotegemea kusafiri kwenda nchi zenye machafuko, kusitisha safari zao hadi hali ya usalama itakaporejea. Ikitokea kuna ulazima wa kwenda huko, tahadhari inatakiwa kuchukuliwa muda wote wanapokuwa kwenye nchi hizo.

**121.** *Mheshimiwa Spika*, ili kurahisisha utoaji wa huduma za Kikonseli ikiwemo kurudisha Watanzania walioko kwenye nchi zenye mapigano, vita au gharika (*Natural Calamities*). Naomba kuchukua fursa hii kwa mara nyingine tena kuwashauri Watanzania wanaoishi au kwenda nje ya nchi kwa shughuli mbalimbali kujiandikisha kwenye Balozi zetu zilizo karibu nao ili waweze kutambulika na kusaidiwa pindi yanapotokea matatizo mbalimbali kama vita na machafuko. Hali hii itasaidia kurahisisha ufuatiliaji wa Watanzania hawa pindi matatizo mbalimbali yanapotokea katika nchi walizopo.

## **MCHANGO WA WIZARA KWENYE SEKTA MBALIMBALI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**122.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na changamoto ya ufinyu wa bajeti, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi nyingine za Serikali na Sekta Binafsi katika kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi yetu. Naomba kwa ruhusa yako, nieleze kwa kifupi mchango wa Wizara kwenye baadhi ya sekta za kijamii na kiuchumi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016). Baadhi ya sekta zilizonufaika na utekelezaji wa diplomasia ya uchumi ni pamoja na Elimu, Afya, Maji, Viwanda, Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Uchukuzi, Biashara, Uwekezaji na Ajira.

## Sekta ya Elimu

**123.** *Mbeshimiwa Spika*, katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa vitabu vya sayansi na hesabu katika Shule za Sekondari, Wizara imeendelea kuwasiliana na wadau wa maendeleo ili kuweza kufanikisha upatikanaji wa vitabu hivyo. Napenda kuliarifu Bunge lako kwamba, tayari Serikali ya Marekani imesaidia Tanzania kuchapisha na kukabidhi vitabu milioni mbili na laki tano vya sayansi na hesabu kwa ajili ya Shule za Sekondari za Serikali. Tunaamini vitabu hivyo vitasaidia kuongeza ari ya wanafunzi na kujenga tabia ya kujisomea. Aidha, nazisihhi Jumuiya za Watanzania waishio ughaibuni na Watanzania wote kwa ujumla waone umuhimu wa kushirikiana na Serikali katika mpango wa kuboresha sekta ya elimu nchini kwa kuchangia vitabu, vifaa vya maabara au kujenga shule za kisasa hapa nchini.

**124.** *Mbeshimiwa Spika*, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Nishati na Madini imeendelea kutafuta fursa za masomo nje ya nchi ili tuweze kuwa na wataalam wa kutosha kwenye sekta ya mafuta na gesi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari tumefanikiwa kupata nafasi za masomo zaidi ya 100 kutoka Serikali ya Watu wa China kwenye sekta ya mafuta na gesi, na sekta nyinginezo. Aidha, Mashirika mbalimbali ya kimataifa na nchi nyingine rafiki zikiwemo Malaysia, Indonesia, Pakistan, Iran, Malta, Egypt, Sri Lanka, Brunei Darussalam, Canada, Ujerumani, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Ubelgiji, Oman, Algeria, Urusi, Australia, Japan na Korea pia zimeendelea kushirikiana nasi katika kuwajengea uwezo Watanzania kupitia ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali.

## Sekta ya Afya

**125.** *Mbeshimiwa Spika*, katika juhudi za kuboresha sekta ya afya nchini, Wizara



yangu iliratibu upatikanaji wa Meli ya *MV Jubilee Hope* kutoka kwa Asasi isiyo ya kiserikali ya *Vine Trust* ya nchini Uingereza. Meli hiyo ya kisasa iliyotolewa na Binti wa Malkia wa Uingereza, *Princess Anne* ambaye ndiye mlezi wa Asasi ya *Vine Trust*, inatoa huduma za afya katika visiwa vyote vilivyopo Ziwa Victoria, hususan vile ambavyo havijafikiwa na huduma za afya.

**126.** *Mheshimiwa Spika*, vilevile, napenda kutumia fursa hii kuzishukuru nchi mbalimbali ambazo zimeendelea kutusaidia madaktari, vifaa vya maabara na tiba, pamoja na kuendelea kuiboresha miundombinu ya afya. Mchango wao huo umekuwa wa msaada mkubwa katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kukabiliana na changamoto ya upungufu wa madaktari sambamba na uboreshaji wa sekta ya afya.

## **Sekta ya Maji**

**127.** *Mheshimiwa Spika*, Tanzania inaishukuru Serikali ya India kwa uamuzi wake wa kuipatia mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 268.35 kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria-Kahama-Shinyanga hadi Tabora-Igunga na Nzega. Mradi huo unaotarajiwa kukamilika mwaka 2016, utatoa huduma ya uhakika ya upatikanaji wa maji ya kutosha katika maeneo husika na unakadiriwa kuwahudumia zaidi ya wakazi milioni moja.

**128.** *Mheshimiwa Spika*, kwa upande mwingine, Serikali hiyo ipo mbioni kukamilisha taratibu za mwisho za upatikanaji wa mkopo wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 92.18 kwa ajili ya miradi ya maji Zanzibar. Mkopo huo utasaidia kuimarisha mifumo ya ugavi wa maji pamoja na mifumo ya kifedha ya Mamlaka ya Maji ya Zanzibar.

## **Sekta ya Viwanda**

- 129.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu inaendelea kushirikiana kwa karibu na taasisi nyingine muhimu nchini katika kuratibu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya China kuhusu kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa Nchi za mfano Barani Afrika katika uanzishaji wa Viwanda. Mpango huu ambao utakwenda sanjari na kubadilishana uzoefu katika uendelezaji wa viwanda ni sehemu ya matokeo ya ziara ya Mheshimiwa Rais Kikwete aliyoifanya nchini China mwezi Oktoba, 2014 na unadhihirisha nia ya dhati ya Serikali ya China ya kufanya kazi na Nchi za Afrika ili kuzisaidia kuleta mapinduzi ya Viwanda na kukabiliana na umaskini.
- 130.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali ya Tanzania inalo jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Mpango huo wa kuleta mabadiliko ya viwanda nchini unafanikiwa. Kwa kuwa mpango huo utagusa sekta zote za kiuchumi, hatuna budi kuweka mikakati itakayohusisha wadau kutoka sekta mbalimbali. Mikakati hiyo itasaidia kuweka uelewa mpana na wa pamoja kwa lengo la kuhakikisha kuwa fursa hii inatumika kikamilifu kwa maendeleo ya taifa.

## **Sekta ya Maliasili na Utalii**

- 131.** *Mheshimiwa Spika*, katika kuongeza jitihada za kupambana na tatizo la ujangili nchini, Wizara imeendelea kupata ufadhili wa vifaa kwa ajili ya mapambano dhidi ya ujangili kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo. Kwa mfano, hivi karibuni Serikali ya Ujerumani ilitupatia msaada wa magari na vifaa vingine katika kuunga mkono jitihada zetu za kupambana na ujangili. Aidha, Wizara yangu imekuwa ikishawishi viongozi mashuhuri wanaofanya ziara hapa nchini kwenda kutembelea baadhi ya vivutio vya utalii tulivyonavyo kwa lengo la kutangaza vivutio hivyo kwa wageni hao na dunia kwa ujumla.

## **Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

- 132.** *Mheshimiwa Spika*, katika kutafuta masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo, Wizara imeendelea na juhudi mahsusi ya kuzitangaza fursa za mazao ya kilimo na mifugo. Mwezi Januari 2015, Wizara kwa kushirikiana na Ubalozi wa Oman hapa nchini, iliandaa Mkutano uliowakutanisha wafanyibiashara wa Tanzania na Oman, ambapo makubaliano kadhaa ya kibiashara yalifanyika. Aidha, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo kwenye hatua za mwisho za utekelezaji wa ushirikiano kati ya Shamba la Mifugo la Dubai (Al Rawabi Dairy Farm) na Ranchi mbalimbali za Tanzania kwa kuanzia na Ranchi ya Mwabuki, Mwanza. Hii ni moja katika hatua muhimu zinazochukuliwa na Serikali kwa ajili ya kufufua na kuboresha Ranchi za Taifa.
- 133.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara ilitibu ushiriki wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Kilimo na Mifugo yaliyofanyika mjini Paris, Ufaransa. Ushiriki katika maonesho haya uliwezesha wataalam wa sekta ya Mifugo na Uvuvi kujionea teknolojia za kisasa zinazotumika kwenye sekta hiyo. Pia waliweza kufanya majadiliano na taasisi za kuendeleza mifugo na wafanyabiashara kwenye sekta hiyo kwa lengo la kuangalia maeneo ya ushirikiano na uwekezaji kutoka Ufaransa ili kukuza sekta hiyo hapa nchini.
- 134.** *Mheshimiwa Spika*, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Vietnam mwezi Oktoba 2014 nchi hiyo imekubali kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji wa mpunga pamoja na ufugaji wa samaki. Kutokana na hatua kubwa waliyopiga wenzetu katika sekta hizo tunategemea kujifunza mengi kwa manufaa ya wakulima wetu na taifa kwa ujumla.

## Sekta ya Uchukuzi

- 135.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi nyingine za umma imefanikisha kusainiwa kwa Mkataba wa Makubaliano ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na Eneo Huru la Uwekezaji baina ya Tanzania, Kampuni ya *China Merchants Holding International* (CMHI) na Mfuko Mkuu wa Akiba wa Serikali ya Oman (SGRF). Kukamilika kwa mradi huu mkubwa kutaifanya Tanzania iwe na bandari kubwa yenye uwezo wa kuhudumia nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini.
- 136.** *Mheshimiwa Spika*, katika hotuba zangu zilizopita niliriarifu Bunge lako Tukufu kuhusu nia ya Serikali ya Japan kujenga barabara za juu (*flyovers*) katika makutano ya barabara za Nyerere na Mandela. Mradi huu utaanza kutekelezwa wakati wowote kuanzia sasa kwani tayari Serikali ya Japan imeidhinisha Bajeti yake na Mkandarasi amepatikana. Vilevile, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za Ujenzi na Fedha na Taasisi nyingine za Serikali inaendelea kufuatilia ahadi ya Serikali ya Korea kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Daraja jipya la Salenda. Daraja hilo linalokadiriwa kuwa na urefu wa takriban kilomita 7.2 litaanzia Hospitali ya Aga Khan mpaka Barabara ya Kenyatta. Ninaamini kwamba kukamilika kwa miradi hiyo kutasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza msongamano wa magari na muda mwingi unaotumiwa na wakazi wa Dar es Salaam kufika maeneo mbalimbali ya Jiji kwa lengo la utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.
- 137.** *Mheshimiwa Spika*, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya Bunge la Bajeti la mwaka jana kuhusu kulishawishi Shirika la Ndege la Emirates kuongeza ndege pamoja na kuleta ndege ya bei nafuu (*budget flight*), napenda kukufahamisha kuwa mwezi Oktoba, 2014 Shirika la Ndege la “*Fly Dubai*” ambalo ni kampuni tanzu ya Emirates ilizindua ndege zake hapa nchini zitakazofanya safari kutoka

Dubai kwenda Dar es Salaam, Kilimajaro, na Zanzibar na baadae Mwanza na Mbeya. Vilevile, katika kipindi hicho, Shirika la Ndege la Emirates limeongeza ndege nyingine na kufanya kuwa na ndege mbili kwa kila siku. Mafanikio haya yatasaidia katika kuongeza watalii nchini, ajira kwa Watanzania na kukuza biashara kati ya Tanzania na UAE pamoja na Nchi za jirani.

## **Biashara na Uwekezaji**

**138.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi nyingine katika kutumia vizuri fursa za ziara za Viongozi wa Kitaifa nje ya nchi na ziara za Viongozi wa Kitaifa wa nje nchini kwa kuratibu Makongamano ya kibiashara na uwekezaji. Makongamano hayo yamekuwa ni fursa ya kuwakutanisha Viongozi wa Serikali na wawekezaji wakubwa kwa lengo la kujenga uhusiano wa kibiashara, kubadilishana uzoefu pamoja na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano. Miongoni mwa Makongamano hayo ni pamoja na Jukwaa la Biashara la Tanzania na Marekani; Uholanzi; China; Ufaransa; Ujerumani; India; Canada; Dubai na Comoro.

**139.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu pia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (BADEA) na Chemba za Biashara za Nchi zote za Ghuba (GCCC), ilifanikisha Kongamano kubwa la Biashara na Uwekezaji lililofanyika mwezi Januari, Jijini Dar es Salaam. Kongamano hilo liliwakutanisha wafanyabiashara wapatao 200 kutoka nchi zote za Ghuba (Kuwait, Qatar, Oman, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu na Bahrain) pamoja na wafanyabiashara wa Tanzania wakiongozwa na Chemba za Biashara za pande zote mbili ambapo makubaliano mbalimbali yalifikiwa.

**140.** *Mheshimiwa Spika*, kwa kupitia makongamano haya, matunda yameanza kuonekana ambapo Kampuni mbalimbali kutoka nchini Marekani, Uholanzi na Ufaransa yamejitokeza na kutembelea Tanzania kujionea fursa zilizopo. Takwimu zinaonyesha katika kipindi cha mwezi Agosti, 2014 hadi Machi,

2015 tayari zaidi ya kampuni 30 kutoka nchi za Marekani, Uholanzi na Canada zimesajiliwa katika Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ambapo inategemewa zitatoa ajira zaidi ya 5,000.

## **Sekta ya Ajira**

- 141. *Mheshimiwa Spika***, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na wadau mbalimbali katika kufanikisha utekelezaji wa Mkataba wa Ajira baina ya Tanzania na Qatar uliosaniwa mwezi Juni, 2014. Hadi hivi sasa kikosi kazi cha wadau kutoka Tanzania na Qatar kinaendelea kuchambua Watanzania wenye sifa kwa lengo la kupelekwa Qatar kufanya kazi mbalimbali hususan katika kipindi hiki ambacho Qatar inaendelea na maandalizi ya Kombe la Dunia la FIFA la mwaka 2022.
- 142. *Mheshimiwa Spika***, Vilevile, Wizara imefanikiwa kulishawishi Shirika la Ndege la Emirates kutenga idadi maalum kwa ajili ya ajira za Watanzania. Tayari Shirika hilo limetangaza ajira kadhaa na usaili umefanyika mwezi Aprili mwaka huu jijini Dar es Salaam.
- 143. *Mheshimiwa Spika***, ni azma ya Wizara kuona kwamba utaratibu kama huo unatekelezwa na Mashirika mengine ya ndege katika kufanikisha jukumu hilo, hivi sasa mazungumzo yanaendelea na Shirika la Ndege la FlyDubai lililoanzisha safari zake hapa nchini hivi karibuni.
- 144. *Mheshimiwa Spika***, mchango huo wa Wizara katika sekta mbalimbali unadhihirisha namna ambavyo uhusiano wetu na wadau wa maendeleo kama vile taasisi za fedha za kimataifa, mashirika na taasisi za kimataifa, na nchi marafiki yanavyoimarika. Aidha, kupitia uhusiano huo mzuri, Wizara imeendelea

kuwashawishi washirika wetu wa maendeleo kutekeleza ahadi zao mbalimbali kwa nchi yetu.

**145. *Mheshimiwa Spika*,** hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote wa maendeleo hususan Taasisi za Kifedha za Kimataifa, Taasisi za Umoja wa Mataifa, nchi wahisani na marafiki pamoja na Asasi mbalimbali za kiraia ambazo zimekuwa zikiunga mkono juhudi zetu za kujiletea maendeleo. Aidha, katika utekelezaji wa diplomasia ya uchumi, Wizara itaendelea kuratibu makongamano ya kibiashara na uwekezaji, kutafuta fursa za ajira kwa Watanzania nje, kushirikiana na nchi marafiki na taasisi hizo katika kuwajengea uwezo Watanzania pamoja na kutafuta masoko ya bidhaa zetu nje.

## **UTAWALA NA MAENDELEO YA WATUMISHI WIZARANI NA BALOZINI**

**146. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kuboresha maslahi ya Watumishi wake. Miongoni mwa maeneo ambayo Wizara yangu imeyapa uzito mkubwa ni suala la mafunzo, kupandishwa vyeo pamoja na uteuzi, na uhamisho wa Watumishi kwenda kufanya kazi katika vituo vyetu vya uwakilishi nje pamoja na kuwarejesha nchini wale waliostaafu na waliomaliza muda wao wa kuhudumu katika vituo hivyo.

### **Mafunzo ya Watumishi**

**147. *Mheshimiwa Spika*,** hivi sasa, Wizara yangu inatekeleza Mpango wa Mafunzo wa miaka mitatu ulioanza katika mwaka wa fedha 2013/2014 na unaotarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2015/2016. Hadi kufikia mwezi Mei 2015, Watumishi 38 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na 32 wanahudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015 imewapandisha vyeo watumishi 70 wa kada mbalimbali baada ya kupokea kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

## Uteuzi wa Viongozi

- 148.** *Mheshimiwa Spika*, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hivi karibuni, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa Watendaji Wakuu wa Wizara yangu ambapo aliwateua Balozi Liberata Rutageruka Mulamula kuwa Katibu Mkuu na Balozi Hassan Simba Yahya kuwa Naibu Katibu Mkuu. Nawapongeza sana kwa uteuzi huo na naamini tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Wizara kwa kipindi kilicho baki.
- 149.** *Mheshimiwa Spika*, vilevile, Mheshimiwa Rais alifanya uteuzi wa Mabalozizi wa Tanzania katika maeneo mbalimbali ya uwakilishi. Wawakilishi hao walioteuliwa ni Balozi Andrew Mugendi Zoka (Ottawa), Balozi Ali Iddi Siwa (Kigali), Balozi John Michael Haule (Nairobi), Balozi Hemedi Iddi Mgaza (Riyadh), na Balozi Rajabu Hassan Gamaha (Bujumbura). Aidha, Mheshimiwa Rais alimhamisha Kituo Mheshimiwa Dkt. Batilda Salha Buriani kutoka Nairobi kwenda Tokyo.

## Kuwarejesha nchini Watumishi waliomaliza muda wao nje

- 150.** *Mheshimiwa Spika*, kwa nyakati tofauti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imekuwa ikielekeza Wizara yangu kutafuta fedha na kuwa na mpango mahususi na endelevu wa kuwarudisha watumishi wastaafu na wale waliomaliza muda wa kufanya kazi Balozini. Zoezi hili limekuwa likikwamishwa na ukosefu wa fedha unaosababishwa na ufynyu wa bajeti.
- 151.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na ufynyu wa bajeti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 tumefanikiwa kuwarejesha nyumbani watumishi wote kumi na sita (16) waliostaafu kati ya hao wamo mabalozizi sita (6). Vilevile, Wizara imepeleka watumishi kumi na wanne (14)



vituoni kuziba nafasi zilizoachwa wazi. Aidha, tumeweka mpango endelevu wa zoezi hili na mikakati ya kupata fedha za utekelezaji wake.

## **Mkutano wa Nne wa Mabalazi wa Tanzania**

**152.** *Mheshimiwa Spika*, baada ya kupita kipindi kirefu bila kufanya Mikutano ya Mabalazi wa Tanzania kutokana na ukata, hatimaye tarehe 25 hadi 27 mwezi huu, Wizara yangu ilifanikisha azma hiyo. Hata hivyo, licha ya kutofanya mikutano hiyo, tuliendelea kuwasiliana na wawakilishi hao ikiwemo kuwapatia maelekezo na miongozo kutoka kwa Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa kuhusu utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje.

**153.** *Mheshimiwa Spika*, Mikutano ya namna hii hutoa fursa kwa wawakilishi wetu pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi nyingine za umma kujadili namna ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na kutoa muelekeo wa Wizara katika kutimiza mipango na mikakati mbalimbali ya Taifa ya maendeleo. Vivyo hivyo, Mkutano wa Nne wa Mabalazi wa Tanzania umekuwa na mafanikio makubwa. Mkutano huo ulitoa maazimio kadhaa kuhusu namna ambavyo Wizara inaweza kuchangia utekelezaji wa mipango na mikakati ya Dira ya Taifa ya Maendeleo inayolenga kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**154.** *Mheshimiwa Spika*, ni matarajio yangu kwamba michango na uzoefu uliopatikana kutoka kwa wadau mbalimbali walioshiriki katika mijadala na mada zilizowasilishwa italetika fikra na mtazamo mpya katika utekelezaji wa Sera ya Nchi ya Mambo ya Nje.

## TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**155.** *Mheshimiwa Spika*, Wizara yangu pia imepewa jukumu la kuzisimamia Taasisi Tatu ambazo ni Chuo cha Dipolomasia (CFR) kilichopo Kurasini jijini Dar es Salaam, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM) na Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC), ambacho pia kinasimamia Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) kilichopo Dar es Salaam.

### Chuo cha Diplomasia

**156.** *Mheshimiwa Spika*, chuo kimeendelea kujiimarisha na kuboresha huduma zake kwa Wizara na umma kwa ujumla. Katika maboresho hayo Chuo kimeongeza programu zake ambapo sasa kimeanza kutoa Shahada ya kwanza ya Uhusiano ya Kimataifa na Diplomasia. Kadhalika, Chuo kipo mbioni kuanzisha Programu ya Shahada ya Umahiri katika fani ya Uhusiano ya Kimataifa na Diplomasia.

**157.** *Mheshimiwa Spika*, Chuo kimesaini Mkataba wa kuanzisha ushirikiano na Chuo cha Mambo ya Nje cha Argentina ambao unaanzisha Programu za kubadilishana Wahadhiri na Wanafunzi, kufanya tafiti za pamoja na kupata walimu wa lugha ya Kihispania kutoka Argentina. Wizara yangu inaendelea kutafuta fursa za ushirikiano wa aina hiyo kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Chuo chetu na vyuo vingine vya Nje.

**158.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu imetenga fedha za maendeleo ili kuboresha miundombinu ya Chuo hicho ili kutekeleza Mpango Kabambe (Master Plan) wa Chuo kwa lengo la kuongeza uwezo na ufanisi wa chuo kudahili wanafunzi zaidi na kujitegemea.

**159.** *Mheshimiwa Spika*, Aidha, Chuo kinaendelea na jukumu lake la kuishauri Wizara yangu katika masuala mbalimbali ya kidiplomasia, kutoa mafunzo maalum kwa watumishi wa Wizara, na kutoa mafunzo kwa Mabalazi wateule na wenza wao.

### **Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora (APRM)**

**160.** *Mheshimiwa Spika*, shughuli inayoendelea kufanyika sasa katika Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora ni kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa (NPoA). Mpango huo uliandaliwa ili kuondoa mapungufu yaliyoainishwa katika Ripoti ya Nchi kuhusu Utawala Bora. Hivyo, APRM imetekeleza majukumu yafuatayo;

- (a) Kuandaa mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kuondoa mapungufu ya utawala bora yaliyobainishwa kwenye Ripoti;
- (b) Kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kuondoa Mapungufu ya Utawala Bora katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali zilizo guswa na Ripoti;
- (c) Usambazaji wa Matokeo ya Ripoti na Uhamasishaji wa Shughuli za APRM Tanzania;

### **Mafanikio ya Utekelezaji wa APRM**

**161.** *Mheshimiwa Spika*, katika utekelezaji wa shughuli za APRM, yafuatayo ni mafanikio tuliyopata;

- (a) Mpango huu unagusa maslahi ya wananchi kwa kiasi kikubwa na umesaidia kutimiza dhana inayoungwa mkono duniani kote ya utawala

shirikishi (*participatory governance*) kwa kuwapa wananchi fursa ya kuishauri serikali yao;

- (b) Mpango huu unazidi kujenga uwezo wa wataalam wetu wa ndani wa kufanya tathmini za utawala bora na hivyo kuwa na hazina ya Wataalam watakaoundeleza usimamizi wa maarifa (*knowledge management*) kwa kufanya tafiti, na kuwasilisha taarifa ya tafiti hizo kwa wadau ili zitumike kuleta ufanisi katika masuala ya utawala bora;
- (c) Kunufaika kwa ushauri kutoka nchi nyingine za Kiafrika zinazoshiriki katika mpango huu, kwa kubadilishana uzoefu katika maeneo yaliyodhihirika kuendeshwa kwa utawala bora, na kusaidiana pale penye changamoto;
- (d) Imekuwa fursa adhimu kwa Serikali kuweza kupata mrejesho juu ya sera, sheria na mikakati mingine inayotekelezwa na Serikali. APRM Tanzania imekuwa kiungo kinachofanya tafiti na kubaini maeneo ambayo Serikali inafanya vizuri na kushauri uboreshaji wa maeneo yenye mapungufu; na
- (e) APRM imeipa nchi yetu fursa ya kuwaonyesha kwa uwazi zaidi wabia wetu wa maendeleo na wawekezaji jitihada zetu za kujikwamua kiuchumi, kijamii na mikakati ya kuimarisha utawala bora. Hivyo, kuongeza imani kwa wawekezaji na kuendeleza heshima ya nchi yetu kimataifa.

## **Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) 2015/16**

**162.** *Mbeshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2014, Kituo kiliweza kuwa mwenyeji wa mikutano ya kimataifa 49 na ya kitaifa 115 iliyoingiza nchini wageni wanaokadiriwa kufikia 37,964. Aidha, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015 Kituo kimeweza kuwa mwenyeji wa Mikutano 149 ambayo 36 ni ya Kimataifa na 113 ya kitaifa.

- 163.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa mara nyingine tena, Kituo kimeendelea kupata hati safi ya hesabu zake zilizoandaliwa na kukaguliwa kwa wakati kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2014. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016, Kituo kimepanga kuingiza mapato ya shilingi 13,748,470,422.00 kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikiwemo Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC), ambacho kilikabidhiwa kwa AICC Agosti 2013. Kipato kinachotegemewa kupatikana kutoka Kituo hiki kipya ni Shilingi 2,551,760,000.00.
- 164.** *Mheshimiwa Spika*, AICC inategemea kukopa Shilingi Bilioni 5 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na mali za kudumu zenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.22. Mikopo hiyo ni kwa ajili ya Miradi ya upanuzi wa Hospitali pamoja na jengo la maonesho. Miradi yote inayotekelezwa imeombewa kibali cha Msajili wa Hazina.
- 165.** *Mheshimiwa Spika*, Kwa kuzingatia upatikanaji wa nafasi baada ya Mahakama ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda (*UN-ICTR*) kupunguza shughuli zake na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (*EAC*) kurudisha baadhi ya ofisi zake na kuhamia kwenye jengo lao jipya, Kituo kitaendelea kupokea taasisi zingine za kitaifa na kimataifa zitakazopenda kuweka makao yake jijini Arusha.

## **MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

- 166.** *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu iliidhinishiwa Bajeti ya Shilingi **190,297,349,000.00** ambapo kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **154,535,649,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi **30,000,000,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi **5,761,670,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara.

- 167.** *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya Shilingi **18,633,022,478.00** ambayo ni mapato yatokanayo na viza zinazotolewa katika Balozi zetu nje.
- 168.** *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara yangu ilipokea kutoka Hazina jumla ya Shilingi **153,779,631,016.00** sawa na asilimia 80.8 ya fedha za bajeti ya Wizara zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2014/2015. Kati ya fedha hizo Shilingi **132,083,323,456.00** ni kwa ajili ya bajeti ya Matumizi Mengineyo, Shilingi **5,040,803,560.00** kwa ajili ya mishahara na Shilingi **16,655,504,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.
- 169.** *Mheshimiwa Spika*, katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali yatokanayo na mauzo ya viza katika Balozi zetu, hadi kufikia kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2015, Wizara yangu imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi **11,518,814,492.00** sawa na asilimia 62 ya makadirio ya makusanyo yote ya Shilingi **18,633,022,478.00** kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, ni matumaini yangu kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2015 ya mwisho wa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu itakamilisha lengo ya ukusanyaji wa maduhuli hayo kama ilivyopangwa.

## **CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

- 170.** *Mheshimiwa Spika*, pamoja na kuwepo mafanikio hayo makubwa ya kiutendaji katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu inakabiliwa na changamoto mbalimbali za kibajeti. Changamoto hizo zimeathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kama ifuatavyo;-

- (i) Baadhi ya Mabalozzi wetu kushindwa kuwasilisha hati za utambulisho na hivyo, kushindwa kuimarisha uhusiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kiusalama n.k.
- (ii) Wizara kushindwa kuwapeleka kwa wakati maafisa wanaopata uhamisho wa kwenda kufanya kazi Balozini (posting) na kushindwa kuwarudisha kwa wakati Mabalozzi na Maafisa waliomaliza kipindi chao cha kufanya kazi Balozini na wale waliostaafu na hivyo Balozzi zetu kuwa na watumishi wachache wanaokabiliwa na majukumu mengi kupita uwezo wao;
- (iii) Wizara kushindwa kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo ya ofisi na makazi yanayomilikiwa na Serikali nje; na
- (iv) Pamoja na Wizara kufanikiwa kupeleka magari 20 kwenye Balozzi zetu mbalimbali bado baadhi ya Balozzi zetu zinakabiliwa na upungufu wa magari ya uwakilishi na huduma Balozini kufuatia kuchakaa kwa magari yaliyopo.

**171. *Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ambazo ni pamoja na kuiomba Serikali kuongeza ukomo wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo na Bajeti ya Maendeleo ili kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**172. *Mheshimiwa Spika***, aidha, kwa kutambua umuhimu wa kupunguza gharama za pango zinazoikabili Serikali katika Balozzi zake, Wizara imeendeleza majadiliano na Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii ya hapa nchini kama vile NSSF, PSPF, LAPF na PPF kwa lengo la kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na Serikali nje ya nchi.

**173.** *Mheshimiwa Spika*, hadi hivi sasa tayari Wizara imeshafanya makubaliano na NSSF ili waanze ujenzi wa mradi wa Kitega Uchumi katika kiwanja cha Serikali kilichopo Nairobi, nchini Kenya. Wizara itaendelea na mazungumzo na mifuko mingine kwa ajili ya kutekeleza miradi mingine katika viwanja vya Serikali vilivyopo Abuja, Lusaka, Maputo, London na Addis Ababa.

## **MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

**174.** *Mheshimiwa Spika*, kwa muhtasari miongoni mwa malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2015/2016 ni pamoja na:

- (i) Kufanya mapitio ya Sera ya Mambo ya Nje na kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara;
- (ii) Kuendelea kurejesha maafisa waliomaliza muda wao katika Balozi za Tanzania pamoja na kuwapeleka wengine kujaza nafasi hizo;
- (iii) Kuratibu Tume za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano (JPC);
- (iv) Kuendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya Umoja wa Mataifa yanayoendelea kuhusu Ajenda ya Maendeleo baada ya mwaka 2015;
- (v) Kuratibu utekelezaji wa makubaliano mbalimbali ya Umoja wa Afrika, hususan Ajenda 2063 ambayo ndiyo dira ya maendeleo ya Bara la Afrika kwa kipindi cha miaka 50 ijayo; na
- (vi) Kuendelea kuongeza uwakilishi wa Tanzania nje kwa kufungua Balozi mpya, Konseli na kutumia Konseli za Heshima sambamba na kuongeza umiliki wa nyumba za makazi na ofisi kwa kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.



## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

- 175.** *Mheshimiwa Spika*, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara yangu imepangiwa bajeti ya kiasi cha Shilingi **154,870,238,000.00**. Kati ya fedha hizo Shilingi **142,870,238,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **12,000,000,000.00** ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo.
- 176.** *Mheshimiwa Spika*, katika bajeti ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara, Shilingi **134,201,251,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **8,668,987,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara. Kati ya fedha za Bajeti ya Matumizi Mengineyo Shilingi **1,130,000,000.00** ni kwa ajili ya Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Tanzania (APRM), Shilingi **3,639,040,000.00** ni kwa ajili ya fedha za Mishahara na Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia na Shilingi **1,304,574,000.00** ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, na Taasisi ya Afrika ya Sheria za Kimataifa.
- 177.** *Mheshimiwa Spika*, katika fedha za bajeti ya maendeleo kiasi cha Shilingi **12,000,000,000.00** zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Shilingi **3,989,121,000.00** zitatumika katika marejesho ya riba ya mkopo wa ujenzi wa jengo la kitega uchumi Nairobi, Kenya; Shilingi **5,115,967,000.00** zitatatumika kukarabati jengo la ofisi na makazi ya Balozi na Mkuu wa Utawala Ubalizi wa Maputo, Msumbiji; Shilingi **2,673,348,000.00** zitatumika kukarabati makazi ya Balozi Stockholm, Sweden; na Shilingi **221,564,000.00** zitatumika kuboresha mfumo wa mawasiliano kati ya Wizara na Balozi za Tanzania nje.

**178.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara yangu kupitia Balozi zake, inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **20,036,019,000.00** kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimejumuishwa kama sehemu ya bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara.

## HITIMISHO

**179.** *Mheshimiwa Spika*, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu yaliyotajwa hapo juu, kwa mwaka wa fedha 2015/2016, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishhe jumla ya Shilingi **154,870,238,000.00**. Kati ya fedha hizo Shilingi **142,870,238,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **12,000,000,000.00** ni kwa ajili ya bajeti ya Maendeleo.

**180.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.





Jengo la Ulinzi na Usalama la Umoja wa Afrika (AU) jijini Addis Ababa lililopewa jina la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kama ishara ya kuenzi mchango wake katika harakati za ukombozi wa nchi za Bara la Afrika.



**Wizara ya Mambo ya Nje na  
Ushirikiano wa Kimataifa**

20 Kivukoni Front  
11466, Dar es Salaam  
S.L.P. 9000, Dar es Salaam  
Tel: +255 (0) 22 211 1906-8  
Fax: +255 (0) 22 226 600  
Email: [nje@foreign.go.tz](mailto:nje@foreign.go.tz)  
Website: [www.foreign.go.tz](http://www.foreign.go.tz)